# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Septemba 6, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580330

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 9



## Mgombea mwenza wa Rungwe anadi kujenga daraja Dar hadi Zanzibar

UKURASA 2

RIPOTI MAALUM

# Wanaofanyiwa 'massage' hatarini

**WATAALAMU** wa MOI wafichua makosa makubwa, watoa huduma hiyo wanena... *Endelea Ukurasa wa 4*



Mgombea Urais wa Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Hashim Rungwe, akinadi sera zake katika uzinduzi wa kampeni za urais, ubunge na udiwani za chama hicho katika eneo la Manzese Bakhresa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO


UKURASA WA 7

**FIKRA MBADALA**

**TUNATAKA KAMPENI ZA KISASA SI KISASI**

KAMPENI kuelekea uchaguzi mkuu nchini zimeanza. Bila shaka, Watanzania, wanasiasa na wasio wanasiasa, wapiga na wapigiwa kura...

UKURASA WA 8

**DARASA LA NDOA**

**NI HAKI NDUGU, KUINGILIA NDOA?**

WATU wengi wanatamani kuoa au kuolewa. Ni jambo jema kwani Mungu alianzisha taasisi ya ndoa ili...


## Gwajima aliamsha 'dude' Kawe

UKURASA 3

# Magufuli aahidi kuongeza mishahara

**NCCR-**Mageuzi yazindua rasmi kampeni ikisisitiza utu, Lissu aisimamisha Mbeya... *Endelea Ukurasa wa. 2*



Mgombea Urais wa Chama cha NCCR-Mageuzi, Yeremia Maganja, akinadi sera zake katika uzinduzi wa kampeni za urais, ubunge na udiwani za chama hicho katika viwanja vya Mbagala Zakhem jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store


MICHEZO **SIMBA, YANGA ZAANZA KUSAKA UFALME LIGI KUU** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Lissu kufuta vitambulisho vya machinga

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ameahidi kufuta utaratibu wa serikali kutoa vitambulisho maalum kwa wafanyabiashara ndogo, maarufu machinga, ikiwa atashinda nafasi hiyo katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Lissu alitoa ahadi hiyo jana kwenye Uwanja wa Ruanda Nzovwe jijini hapa wakati wa mkutano wa uzinduzi wa kampeni za chama hicho Kanda ya Nyasa, akiahidi kujenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za kundi hilo ambayo yatakuwa wazi usiku na mchana.

Lissu alisema baadhi ya wananchi huwa wanachelewa kufika kwenye miji yao wanapokuwa wametoka safarini na hivyo kukosa huduma za kununua mahitaji kwenye masoko kutokana na masoko hayo kufungwa kwa kisingizio cha usalama.

"Tutafuta utaratibu wa kuwauzia wamachinga vitambulisho ambavyo vinatolewa sasa. Pamoja na kupewa vitambulisho hivyo, wanauza bidhaa zao kwenye mitaro na barabarani, jua linakuwa lao na mvua yao.

"Tutajenga masoko maalum kwa kushirikiana na sekta binafsi kwenye maeneo mbalimbali ili machinga wetu wafanye biashara hapo kwa uhuru na kila mmoja atakuwa na chumba chake," aliahidi.

Vilevile, Lissu alisema serikali yao itajenga majengo maalumu kwenye maeneo ya stendi za mabasi kwa ajili wa wauzaji vyakula, maarufu mamalishe na babalishe, ili wafanyie biashara zao huko kwa uhuru.

Mgombea huyo pia aliahidi kuwa serikali yake haitakuwa ya kulipa kisasi kwa mtu yeyote na badala yake atahunda tume ya maridhiano ambayo itakuwa kwa ajili ya upatanishi wa Watanzania na viongozi wote ambao walifanya makosa watatakiwa kukiri makosa yao na watasamehewa.

Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, alivitaka vyombo vya dola na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuvitendea haki vyama vyote vya siasa wakati huu wa uchaguzi.

Alisema NEC inapaswa kutenda haki hiyo kwa kuwarejesha kwenye mchakato wagombea ubunge na udiwani wa vyama vya upinzani walioenguliwa na baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi.

# JPM aahidi kupandisha mishahara

**Na Gwamaka Alipipi,** MUSOMA

MGOMBEA urais kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, ameahidi kupandisha mishahara ya watumishi wa umma ndani ya miaka mitano ijayo ikiwa atashinda tena kuongoza nafasi hiyo.

Amesema hakutekeleza ahadi hiyo katika kipindi cha miaka mitano ya utawala wake kwa kuwa alitaka kukamilisha kwanza baadhi ya mambo muhimu ya kitaifa ikiwamo ujenzi wa hospitali, zahanati, huduma ya elimu na miradi mingine ya maendeleo.

Alitoa ahadi hiyo jana wilayani Musoma mkoani Mara wakati akiwahutubia wananchi na wanachama wa CCM waliojitokeza katika Uwanja wa Mukendo kumsikiliza.

"Ninawaahidi wafanyakazi, kabla sijaondoka madarakani nitahakikisha nimeongeza mishahara yenu... sikutaka kuongeza awali kwa sababu kuna baadhi ya vitu ilibidi tukamilishe kwanza ndipo lifuate," alisema.

Dk. Magufuli alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano, idadi ya watumishi waliaojiriwa ni 61,000, na serikali yake imelipa maslahi yao, pensheni na malimbikizo zaidi ya Sh. bilioni 200.

"Mtu anakuja anasema hatupandishi mishahara ya wafanyakazi, hivi ukimpandisha mtu daraja, mshahara wake unabaki palepale?

"Masuala ya kuongeza mshahara halafu unapandisha nauli, bidhaa, hapana! Tuliamua kwanza kutoa elimu bure na kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu Sh. bilioni 450 (kwa mwaka). Tungeweza kuwadanganya wafanyakazi tumepandisha mshahara, tuliamua kuanza kusomesha watoto wa maskini bure.

"Ndiyo maana katika hii Ilani ya CCM inazungumzia maslahi ya wafanyakazi, wakulima, wavuvi na kwa wafanyabiashara. Ilani hii inawapenda sana, tumewajali wafanyabiashara wadogo, miaka ya nyuma ukisimama mgambo anakuja kukusumbua," alisema.

Dk. Magufuli pia aliwaahidi Watanzania kuwa atatekeleza mambo aliyoyapanga Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere ndani ya miaka mitano kwa kasi kubwa.

Vilevile, alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo ya utawala wake, atahakikisha kila Mtanzania anakuwa na bima ya afya.

"Hata suala la bima Tanzania tuko mbele sana, katika mipango ya baadaye tunataka kutoa bima kwa watu wote. Ukurasa wa 136 wa Ilani ya CCM inazungumzia kuimarisha mfumo wa afya nchini ikiwamo huduma ya CHF na NHIF. Mtakapotuchagua, tunataka kuipanua kwa Watanzania wote na wakati huo tutakuwa na Watanzania milioni 60," alisema.

Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, amejenga hospitali za wilaya za Bunda, Butiama, Musoma, Musoma, Rorya, Serengeti na Tarime pamoja na vituo vya afya vinane na zahanati 27 kwa Sh. bilioni 25.1.

Alisema serikali yake pia imejenga shule za sekondari 35 na za msingi 102, ujenzi wa nyumba 152 za walimu, ukarabati wa vyuo vya walimu na kutoa Sh. bilioni 49.95 mkoani Mara.

Kwenye sekta ya maji, Dk. Magufuli alisema miradi 38 imetekelezwa kwa Sh. bilioni 68.4. Kati yake, miradi 17 imekamilika huku mingine ikiwa katika utekelezaji.

Mgombea huyo wa CCM pia alisema vijiji 411 mkoani Mara vimefikiwa na huduma ya umeme kati ya 458 kwa gharama ya Sh. bilioni 105.4.



Mjane wa Baba wa Taifa, Mama Maria Nyerere, akisalimiana na Mgombea Urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama hicho, Dk. John Magufuli, wakati wa mkutano wa hadhara wa kampeni za uchaguzi mkuu katika uwanja wa Mkendo, mjini Musoma, Mkoa wa Mara jana. **PICHA: IKULU**

# CHAUMMA yaahidi kujenga daraja Dar hadi Zanzibar

**Na Thobias Mwanakatwe**

MATUMAINI ya wananchi kupata ubwabwa na kuku wakati wa mikutano ya kampeni ya Mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Hashimu Rungwe, yameyeyuka baada Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU) kupiga marufuku utaratibu huo.

Vilevile, chama hicho kimeahidi kujenga daraja kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar ili wananchi waachane na usafiri wa meli na boti ambao kimesema siyo rafiki kwao.

Jana, katika uzinduzi wa kampeni za chama hicho eneo la Manzese Bakhresa jijini Dar es Salaam jana, Rungwe hakutekeleza ahadi yake ya kutoa ubwabwa kwa wananchi kutokana na amri hiyo ya TAKUKURU aliyopewa juzi.

Taasisi hiyo nyeti ilionya kuwa kutoa chakula kwa wananchi kipindi hiki cha kampeni ni kosa kwa mujibu wa sheria. Rungwe alisema jana kuwa alipanga kutoa ubwabwa kwenye mkutano, lakini TAKUKURU wamempiga marufuku.

"Nilipanga chakula kije hapa kwenye mkutano, lakini TAKUKURU wamenikataza, hii roho mbaya tu," alisema Rungwe huku akionyesha kwa wananchi nakala ya Gazeti la Nipashe toleo la jana ambalo lilikuwa na habari ya TAKUKURU kumpiga marufuku mgombea huyo kugawa ubwabwa.

Rungwe alisema inashangaza TAKUKURU kuona suala la kutoa chakula ni rushwa wakati wakialikwa kwenye vikao mbalimbali vinavyoandaliwa na serikali ya CCM wanapewa chai, chakula na mshiko.

Alisema serikali yake itahakikisha inaongoza kwa utawala wa haki na kwamba wananchi watakaovunjia nyumba zao, watalipwa fidia tofauti na sasa ambapo hawalipwi.

"Sisi tunataka utawala wa haki, watu wafanye siasa za haki bila kuonewa," alisema na kuongeza kuwa serikali yake itatoa ajira kwa vijana kwa kuanzisha viwanda.

Mgombea mwenza, Mohamed Masoud Rashid, alisema sera za CHAUMMA ni bora kuliko chama kingine cha siasa nchini na mpango wao wa kupeleka bahari Dodoma wana imani utaporwa.

"Dodoma tangu itangazwe kuwa makao makuu ya nchi imechukua zaidi ya miaka 40 kuhamishia ofisi huko. Kwa hiyo, na sisi tumedhamiria kuipeleka bahari Dodoma ili kuunga juhudi hizo," alisema.

Rashid pia alisema wananchi wakikipa ridhaa chama hicho, serikali yake itajenga daraja kutoka Zanzibar hadi Dar es Salaam ili kurahisisha usafiri.

# Mkumbo aahidi neema Ubungo

**Na Halfani Chusi**

MGOMBEA ubunge wa Ubungo (CCM), Profesa Kitila Mkumbo, amezindua kampeni zake kwa kuomba achaguliwe, akitaja vipaumbele vyake sita ambavyo anaamini utekelezaji wake utawapa raha wananchi wa jimbo hilo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hizo kwenye viwanja vya EPZ vilivyoko Kata ya Makuburi, Profesa Mkumbo alisema ameandaa mipango ya kuboresha hali ya watu wa Ubungo kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi wenyewe.

"Mimi nimekaa Ubungo kwa zaidi ya miaka 20 na hivyo ninaijua vizuri sana. Lakini, kabla ya kuamua kugombea, nilifanya utafiti wa nini hasa wananchi wanataka na baada ya utafiti huo ndiyo nimekuja sasa na mipango ya kuondoa kero hizo," alisema.

Alisema wananchi wengi wa Ubungo wanalalamika kuhusu ukosefu wa barabara nzuri kwenye mitaa wanakoishi, jambo alilolieleza kama kero namba moja, namba mbili na namba tatu ya watu wa jimbo hilo.

Profesa Mkumbo aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kabla ya kuamua kujitosa kwenye ubunge, aliwafurahisha wananchi waliojitokeza kwa kutoa mifano halisi ya kero zao.

Alisema jimbo hilo pia linakabiliwa na tatizo la ukosefu wa mitaro ya majitaka na uchafu wa kwenye masoko, jambo alilosema litaondolewa kwa mipango madhubuti.

"Nimepiga hesabu za haraka haraka hapa na nimeona mamilioni ya shilingi yaliletwa hapa kupitia mfuko wa jimbo, lakini sijui hata zilifanya kazi gani. Nikiwa mbunge, fedha hizo zitatumika vizuri," aliahidi.

Kero nyingine ambazo Profesa Mkumbo aliahidi kupambana nazo endapo atashinda kuwa mbunge ni kupatikana kwa mikopo ya kinamama, vijana na wanaume wanaohitaji, kuboresha upatikanaji wa maji, elimu, kutambua biashara zisizo rasmi na kukuza michezo.

Alisema atajenga ukumbi mkubwa kwa ajili ya shughuli za wasanii na ataboresha masoko yaliyopo na kujenga mapya, kukarabati shule na kujenga shule mpya kwa ajili ya kidato cha tano na sita.

Profesa Mkumbo pia aliahidi kupanua fursa za ajira kwa wananchi wa jimbo hilo, akibainisha kuwa lina miradi miradi mingi ambayo inaweza kuwa fursa kwao kujipatia ujira.

"Pia, tutawapa nafasi wawekezaji wakubwa katika jimbo ili, wakishawekeza nitawashawishi ajira hizo kipaumbele cha kwanza kiwe kwa wanajimbo," alisema.

Jimbo la Ubungo limekuwa mojawapo ya ngome za upinzani katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, likiongozwa na wabunge kutoka Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Katika uchaguzi wa mwaka huu, Profesa Mkumbo anachuana na Meya wa Ubungo aliyemaliza muda wake, Boniface Jacob, ambaye hata hivyo amewekewa mapingamizi.

# NCCR yaanika vipaumbele 10

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi, kimezindua kampeni zake za uchaguzi mkuu wa mwaka huu, kikiainisha vipaumbele vyake 10 kama kitachaguliwa kushika dola, ikiwamo kuzingatia utu na usawa wa kijinsia.

Tukio hilo lililoambatana na uzinduzi wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho iliyopewa jina la 'Mwafaka wa Kitaifa', lilifanyika kwenye Viwanja vya Mbagala Zakhem jijini Dar es Salaam jana.

Katika uzinduzi huo, Katibu Mkuu wa chama hicho, Elizabeth Mhagama, alisema ilani imefanyiwa utafiti na imejibu matatizo mengi yanayoikabili nchi.

"Ni Ilani ambayo inalileta taifa letu kuwa moja, imetokana kwa kuangalia rasimu ya Jaji Warioba, na imefanyiwa utafiti. Nia ya kuandika katiba mpya tunayo na uwezo tunao," alisema Mhagama.

Vipaumbele vya chama hicho ni pamoja na kuufufua mchakato huo wa katiba mpya na kuboresha sekta ya elimu kwa kuwa na falsafa ya elimu ifaayo kwa nchi.

Vingine ni mwafaka wa kitaifa utakaohusu maridhiano juu ya maadili ya kitaifa, kuimarisha na kuboresha afya na ustawi wa jamii, kuboresha mazingira na makazi kwa wananchi, ustawi wa vyombo vya habari na asasi zisizo za kiserikali na kuimarisha usawa wa kijinsia kwa kuhakikisha kunakuwa na idadi sawa ya wanaume na wanawake katika vyombo vya uwakilishi.

Kwa mujibu wa ilani hiyo, vipaumbele vingine vya chama hicho ni kuimarisha uchumi, ulinzi na usalama na kupiga vita dhidi ya rushwa kwa kutengeneza vyombo vyenye nguvu kubwa na mtandao mkubwa wa kuvidhibiti.

Mwenyekiti wa chama hicho, James Mbatia, alisema wameweka misingi ya mwafaka wa kitaifa kwa sababu kumeanza kuonyesha dalili za baadhi ya watu kujionyesha wao ni bora kuliko wengine.

Mbatia alisema anakumbuka wosia ulioachwa na aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, wa kuhakikisha uchaguzi wa mwaka huu unakuwa huru na haki. "Mzee huyu alituachia wosia mzuri wa kuifanya Tanzania inakuwa sehemu nzuri ya kuishi, tuheshimu wosia huu wa mzee aliotuachia," alisema. Mgombea wa urais kwa tiketi ya chama hicho, Yeremia Maganja, alisema akiingia madarakani, atawaita Rais John Mafufuli, Bernard Membe, Profesa Ibrahim Lipumba, Tundu Lissu na Maalim Seif Sharif Hamad katika meza ya maridhiano ya kitaifa.

Maganja pia alisema akiingia madarakani, ndani ya miezi 12 hadi 18, atakuwa amewapatia Watanzania katiba mpya.



Mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu akiwapungia mkono wanachama na wafuasi wa chama hicho, alipowasili katika viwanja vya Nzovwe, jijini Mbeya jana, kwa ajili ya mkutano wa hadhara wa kampeni za uchaguzi mkuu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Gwajima 'aliamsha' Kawe

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAKATI kampeni zikiendelea kupamba moto, Mgombea Ubunge wa Kawe (CCM), Askofu Josephat Gwajima, ameahidi kununua greda na maroli kwa fedha zake ili kutengeneza barabara za mitaa yote ya jimbo hilo ikiwa atashinda katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Pia, amesema atanunua magari ya wagonjwa na kuyasambaza jimboni ndani ya siku 90 baada ya kuchaguliwa, akitamba kuwa hahitaji kusubiri bajeti ya serikali.

Askofu Gwajima alitoa ahadi hizo juzi wakati akizungumza na wanachama wa CCM na wananchi wa Kata ya Kawe alikokuwa anaendelea na mikutano yake ya kampeni.

"Mimi sijaja kufanya kazi hii kuganga njaa, acha hao wa upande ule ambao wanaomba ubunge kutumia fedha waliyokopa benki halafu baada ya miaka mitano wanaanza kurejesha marejesho na mpaka amalize marejesho atakuwa hana muda wa kukuletea maendeleo. Mimi sina marejesho ya kurejesha," alitamba.

Askofu Gwajima aliahidi kuwa baada ya kununua greda na maroli hayo ambayo yatatoa ajira kwa vijana wa Jimbo la Kawe, atahakikisha kila barabara ya mtaa inafanyiwa matengenezo na hivyo kumaliza tatizo la barabara katika jimbo lote.

Mgombea huyo aliahidi kununua magari ya wagonjwa kwa ajili ya jimbo hilo, akidai kuwa hata kabla hajawa mbunge, wapo rafiki zake ambao ni wabunge aliwasaidia kununua magari 18, hivyo kwa Jimbo la Kawe, ununuzi wa magari hayo ni jambo dogo sana kwake.

Askofu Gwajima alisema kabla hajafikiria hata kugombea ubunge, alishasaidia watu zaidi 250 na misikiti saba kwa kuwaunganishia maji katika eneo la Salasala kwa gharama zake.

Askofu Gwajima alisema yeye kugombea ubunge kupitia CCM hakujatokea kwa ajili ya kuuza sura wala kuchoma mahindi, bali ni kwa ajili ya kufanya kazi za kuwaletea maendeleo ya kweli wananchi.

RIPOTI MAALUM

# Tahadhari wanaofanyiwa 'massage'

## ■Mtaalamu wa MOI atoa angalizo

Na Romana Mallya

INAAMINIKA kwamba, namna bora ya kuondoa msongo wa mawazo na uchovu wa mwilini ni kufanya 'massage', yaani kuchua kwa kugusa au kusugua kwa vidole maeneo yenye maumivu.

Massage kwa sasa ni moja ya huduma ambazo zimeshamiri maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, hususan kwenye saluni za wanaume na wanawake.

Hata hivyo, uchunguzi wa Nipashe jijini uliohusisha mahojiano na baadhi ya wanaotoa huduma hiyo, umebaini kwamba wanaopendelea zaidi kupata huduma hiyo ni wanaume kulinganishwa na wanawake.

Je, uchuaji huo ni salama kwa afya? Katika kudadisi usalama wa huduma hiyo, Nipashe ilimtafuta Mtaalamu wa Tiba Mazoezi kutoka Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Lucas Machage, ambaye aliweka wazi kuwa uchuaji unaoendelea kwenye mitaa mbalimbali ya Jiji na maeneo mengine nje ya hospitali, haulengi tiba.

"Haufuati misingi inayotakiwa. Baada ya kuona vurugu hiyo kwa upande wa hospitali, hatuandiki 'massage; bali 'Soft Tissue Mutilation' (unyambuaji wa misuli) na hili linaweza kutimia tu kama mtu amejifunza utaalamu wa uchuaji mahali panapostahili," alisema.

Mtaalam huyo alibainisha kuwa zipo aina nyingi za uchuaji wa mwili zikiwamo za kutumia mikono kutoka sehemu moja ya mwili kwenda nyingine, uchuaji wa kukunja ngozi na uchuaji wa kutumia mikono ikiambatana na mtetemeko fulani.

"Kumbe kuna lengo kwenye kuchua na yapo mambo ya kuzingatia kitaalamu ili kupata matokeo. Matokeo hayo lazima ufuate muundo wa mwanadamu alivyoumbwa.

"Kila msuli kwenye mwili wa mwanadamu umewekwa kwenye nyumba yake, hakuna msuli uliokaa mahali ambako siyo pake, msuli unapofanya kazi unahama sehemu yake," alisema.

Machage alifafanua hoja yake, akieleza kuwa mtu anaponyanyua mikono yake juu, misuli yake inakuwa imehama eneo lake inapopaswa kuwa kama hajishughulishi na jambo lolote.

### MAKOSA YA UCHUAJI

"Mtu akiwa anachua akiwa amelala kitandani, anatakiwa ahakikishe viungo vya mwili wake vinakaa kama vile Mungu alivyoviumba," anasema na kufafanua zaidi kwamba:

"Ukiweka mikono juu ya kichwa, tayari umehamisha msuli eneo lake, ukimchua katika hali hiyo, unakuwa unakandamiza misuli katika mabonde ambayo siyo yake."

Alisema kwa kufanya hivyo utamsababishia maumivu mhusika na hatapata matokeo ya kile alichokuwa amekilenga, hivyo kutotatua tatizo alilonalo.



"Unapomchua mtu kwa kulenga tiba, lazima uzingatie uumbaji wa mwanadamu. Binadamu anaanza kichwa hadi miguu. Wakati unamchua lazima ufuate mtiririko huo, lazima utoke chini kwenye miguu kwenda juu kichwani na siyo kichwani kuja miguuni.

"Kama mtu anataka kuchua kuanzia kiunoni kwenda miguuni, mchuaji anatakiwa kuanzia miguu ili apeleke maji kwenye moyo na uchuaji wa mkono unatakiwa kuanzia kwenye vidole kwenda kwenye bega na wale wa mgongo anatakiwa kuanzia kiunoni kwenda juu," alielekeza.

Alionya kuwa endapo wachuaji wakifanya tofauti na uumbaji wa mwanadamu, madhara yake ni pamoja na kuhamisha misuli kwenye eneo lake na kusababisha maumivu kwa mhusika.

Vilevile, alisema mchuaji anatakiwa wakati akichua, asitumie nguvu nyingi bali aanze na mkandamizo mdogo na akibaini mhusika akikunja uso, anatakiwa kupunguza.

### MUDA WA KUCHUA

Mtaalamu huyo alibainisha kuwa, kitaalamu muda wa ni dakika 30 na ili mtu apate matokeo chanya, lazima uchuaji uwe mwepesi na ufuate misingi ya mhusika kulala katika utaratibu sahihi, kuchua kutoka chini kwenda juu, mkandamizo mdogo na matumizi ya vidole au kiganja kulingana na eneo.

Akizungumzia hatari ya magonjwa ya kuambukiza wakati wa kuchua, mtalaamu huyo alidokeza kuwa uchuaji wa 'massage' zinafanywa na kusababisha msisimko wa maeneo mengine ambayo siyo lengo la uchuaji.

"Ndiyo maana ninasema uchuaji wa mtaani unafanywa mpaka kwenye maeneo ya siri wakidai ni uchuaji, mwisho wa siku unaweza kuleta athari nyingine za kiafya kama maambukizi ya magonjwa," alionya.

Alibainisha kuwa ipo hatari ya kuambukizana magonjwa ikiwa anayefanyiwa ana vidonda au vipele na mfanyaji ana mchubuko kwenye kiganja.

"Uchuaji wa tiba ni lazima mtu afanyiwe vipimo baada ya mtaalamu wa afya kusikiliza historia ya mtu na maeneo anayolalamikia kuchua kwa sababu unaweza kumsababishia mtu matatizo ya kiafya.

"Viungo vya mwili vinaweza kuuma, labda mtu ana malaria au ana shida nyingine mwilini, mtu wa namna hii hahitaji tiba ya kuchua," alisema.

Mtaalamu huyo wa MOI alisema mchuaji lazima ajue eneo husika lenye tatizo na vitu gani atatumika ili kuleta matokeo chanya na siyo kuchua kwa hisia kwa kumsikiliza tu mteja.

"Huwezi kumchua mtu mahali ambako amevunjika, kuna vidonda, uvimbe au mtu ameumia leo halafu kesho akachuliwa au mgongo uliangukiwa na kitu halafu ukamchua. Kuchua kunafanyika kwenye tatizo sugu, lakini tu kama hakuna uvimbe," alionya.

Alifafanua kuwa kuchua eneo lenye uvimbe, kunasababisha kuleta maji mengi na kusababisha uvimbe husika uongezeke.

"Kuchua kwa tiba mtu anaweza kufanya mara 12 kwa mwezi inatosha au mara tatu kwa wiki, ukishindwa hivyo unaweza kufanya kwa kufululiza na baadaye ukapunguza mara tatu au mara moja na ukamaliza," alisema.

Alitaja njia nyingine ya kuchua ni ya kumwekea mhusika mfuko wa maji ya moto eneo husika kwa muda wa dakika kati ya 10 na 15 na baadaye akapakwa mafuta maalum ya maumivu.

"Ushauri wetu kwa wale wanaotaka huduma ya kuchua wawaone kwanza wataalamu wa tiba ya mazoezi, ili wawakague kama shida zao zinahitaji kuchuliwa au la na ni wakati gani wafanyiwe huduma hii.

"Kuna matatizo mengine hayahitaji kuchua wala kuwekewa maji ya moto, unaweza kuweka barafu tu na kupona kwa sababu tatizo ni la muda mfupi siyo la muda mrefu," alisema.

Mtaalamu huyo pia aliwashauri watoa huduma hiyo mtaani kuvaa glovu ili kutoambukizana magonjwa.

### WATOA HUDUMA

Katika udadisi wake, Nipashe ilizungumza na mfanyakazi wa saluni ya kiume ya Nevada iliyoko Sinza jijini Dar es Salaam, Angel Lyimo, ambaye alibainisha kuwa wamekuwa wakipokea wateja wengi na akakiri kuwapo kwa dosari katika kujua hali za afya zao.

"Wapo wanaokuja wakiwa na vipele au chunusi usoni au mwilini na shughuli zetu za saluni zinahusu ngozi, hivyo usipokuwa makini unaweza kuingia kwenye hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa ya ngozi au yatokanayo na mchubuko kama Ukimwi.

"Vifaa vinavyotumika kunyolea unaweza ukakishika vibaya kikakukata, nikipata jeraha, nisiendelee na kazi? Hapana, tunachofanya ni kuchukua tahadhari kubwa ikiwa ni pamoja na kumweleza ukweli mteja," alisema.

Lyimo alisema tahadhari wanazochukua siyo tu kwa mteja ambaye anaonyesha ana harara mwilini au chunusi, bali wakati wote hukikisha wanajali afya zao na za mteja wanayemhudumia.

"Binafsi, bado ni binti mdogo mwenye majukumu ndiyo maana nipo hapa. Siwezi kuhatarisha maisha yangu, ninachukua tahadhari. Hii ni kwa upande wa mteja anayefika hapa kutaka kufanyiwa 'scrub' (kusugua) ambayo inahitaji umsugue eneo husika kuondoa uchafu mwilini," alisema.

Mfanyakazi kazi huyo wa saluni alisema mteja anayetaka huduma ya kusuguliwa uso au mwili, kama atakuwa na chunusi mara nyingi hupewa ushauri tu wa aina ya vipodozi vya kutumia ili kuondoa tatizo na huwa hawamsugui.

"Ila ipo njia ya pili ya kutumia kifaa maalum cha kufukiza ambacho mteja mwenye chunusi badala ya kusugua kwa mkono atapakwa vipodozi vya kuondoa uchafu na kuwekwa kwenye kifaa hicho," alisema.

Kuhusu elimu ya kuchua, Lyimo alisema alijifunza kutoka kwa mtu mtaalamu wa kutoa huduma hiyo aliyeko Magomeni na sasa ana miaka saba na hajawahi kupata malalamiko ya mteja kuwa amepata tatizo la kiafya.

"Tatizo kubwa kwenye kazi yangu, mimi ni msichana na wateja wengi wanaokuja hapa ni wanaume wa rika tofauti na unaweza kufanya kazi yako vizuri, lakini akakutaka kimapenzi.

"Na ukumbuke huduma hii mnaifanyia kwenye chumba maalum ila nikikutana na kitu hiki, ninajaribu kumwelimisha mteja kwa sababu kazi yangu ninaipenda. Wapo ambao wanaingia kwenye kishawishi na kutembea na wateja na hapo hujui afya yake kwa ujumla," alionya.

Yasini Mwinyi, mfanyakazi wa saluni ya kiume ya Family iliyoko Sinza Mori jijini, alisema wanapomwona mteja ana fangasi za miguu au chunusi usoni, huchukua tahadhari kwa kumhudumia kwa kutumia vifaa vipya kwa gharama yake.

"Tunaponunua vifaa hivyo vitatumika kwa ajili ya mteja husika. Kwa ujumla, baadhi ya huduma mfano 'pedicure' vifaa vyake tunapenda mteja anunue, vifaa ni Sh. 10,000 na huduma yenyewe ni Sh. 15,000," alibainisha.

Kuhusu huduma za kuchua mwili, Mwinyi alisema hutozwa kwa saa, kila dakika moja ni Sh. 1,000 na hufanywa kwa ngozi ambayo ni rafiki, kwa maana kwamba haina tatizo.

"Wanaofanya kazi ya kuchua wana elimu ya kujua ni maeneo gani yanatakiwa kuguswa na ambayo hayatakiwi, kwa sababu kwenye mwili wa binadamu kuna mishipa ambayo haitakiwi kuguswa, kama siyo mtaalamu unaweza kuuvunja na kumsababishia ulemavu," alisema.

Mwinyi alisema wanajilinda dhidi ya maradhi ya kuambukiza kwa kutoa ushauri kwa wateja ambao wanawaona ngozi zao siyo rafiki kufanyiwa huduma hiyo.

# Maono ya mbali, sera vinavyompaisha JMP kinyang'anyiro uchaguzi wa urais

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPENI za uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani zimeanza kwa kasi huku wagombea wakichuana kwa hoja, ubunifu na uwezo wa kushawishi wapigakura na vyama vya siasa na wagombea kunadi ilani na sera zao wachaguliwe ifikapo Oktoba 28, mwaka huu.

Lakini pia kipindi hiki ni mahususi kwa wapigakura kutumia sanduku la kura kuwazawadia wanasiasa waliofanya vizuri na kuwaadhibu walioshindwa kutekeleza ahadi zao kutokana na kuchaguliwa kwao.

Kampeni za mwaka huu zimeanza kwa mbwembwe nyingi zilizoambatana na kaulimbiu kama Tutaleta ubwabwa kuku' (CHAUMA) na Kazi na Bata (ACT-Wazalendo), Uhuru, Haki na Maendeleo (CHADEMA).

Lakini mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli (pichani), kwa ujasiri mkubwa, ameibuka na kaulimbiu inayosomeka; 'Tumetekeleza kwa Kishindo, Tunasonga Mbele Pamoja'.

Kampeni za uchaguzi huu si kwamba zinafanyika katika muktadha mpya, bali ni mwendelezo wa kilichoanza mwaka 2015. Kipindi kama hiki miaka mitano iliyopita, CCM, vyama vya upinzani chini ya mwavuli wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) na Anna Mghwira (sasa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro) akipeperusha bendera Chama cha ACT Wazalendo, walipambana vikali katika majukwaa ya kisiasa kunadi sera ya mabadiliko.

Miaka mitano imepita kwa kasi ya mwanga na sasa vyama vimekuja tena kufanyiwa tathmini na wapigakura. Katika wiki ya kwanza ya ufunguzi wa kampeni, vyama vikuu karibu vyote, vimezindua ilani zao na kunadi sera zao kwa umma.

Kitu ambacho wapinzani wa CCM wanashindwa kukiri kwa uwazi ni kuwa haikutarajiwa kama Tanzania ingeendesha uchaguzi katika mazingira huru kama ilivyo sasa kutokana na tishio la janga la corona lililolikumba taifa na dunia miezi kadhaa iliyopita.

Wapinzani walishawahi hata kususia vikao vya Bunge wakiituhumu serikali kutolichukulia hatua stahiki janga hili. Katika tweet yake ya Mei Mosi, mwaka huu, mgombea urais wa CHADEMA, Tundu Lissu aliandika kuwa: "Mheshimiwa Rais Magufuli. Utake usitake, Urais wako wa miaka mitano utaamuliwa na coronavirus na kauli na matendo yako kwenye janga hili! Kwa hiyo tumia wakati huu ukiwa mafichoni Chato kuandaa majibu juu ya 'kaugonjwa kadogo' haka na juu ya vifo hivi vinavyoendelea kuongezeka". Huenda ndugu Tundu Lissu ameisahau tweet hii.

Ni hakika kwamba hakuwa pekee yake katika hofu hii bali kuna Watanzania wengi walikuwa katika taharuki kubwa. Lakini katika hali hiyo tete, Rais Magufuli alionyesha ukomavu wa kiuongozi, maono ya mbali, ujasiri na uthabiti wa kiuamuzi, kuwaelekeza wananchi kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kujenga uchumi wa nchi na kipato binafsi; kushinda hofu ya ugonjwa wa corona na kuhimiza maombi maalum kwa Mwenyezi Mungu.

Si kwamba corona imeisha, lakini sasa, wanasiasa hawa hawa wanashindana kuonyesha uwezo wa kuvutia umati kwenye mikutano yao ya kampeni badala ya kuzingatia 'social distance' kama moja ya mbinu zilizoelekezwa kujikinga na corona.

Maono hayo yanampa Rais Magufuli alama ya vema juu ya maono ya mbali na uthabiti wa kiuongozi alivyoshughulikia suala hilo mpaka sasa na taifa liko huru kuendesha kampeni zenye mikusanyiko mikubwa.


Kwa muktadha wa sera, kaulimbiu ya Ubwabwa Kuku ya Hashim Rungwe wa CHAUMA ni kinyume cha sheria, kwani zinarudisha vitendo vya takrima ambavyo ni rushwa ya uchaguzi zilizofutwa katika hukumu ya kesi maarufu ya Takrima ya Mwaka 2005.

Katika suala la maakuli, Rais Magufuli anajigamba katika Ilani ya CCM kuwa kuongeza uzalishaji wa chakula kutoka tani milioni 15.5 msimu wa mwaka 2015/16 mpaka milioni 16.9 mwaka 2018/19 wakati mahitaji halisi ya nchi ni tani milioni 14.

Wagombea wote wa ACT- Wazalendo na CHADEMA wamezungumzia kuhusu uvunaji wa rasilimali za taifa, yaani madini na gesi. Lissu alidhihaki jitahada za seriakli ya Rais Magufuli kushughulikia sekta ya madini, akihoji kuhusu ankara ya kodi ambayo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) iliwaandikia Accacia katika sakata la makinikia ambapo thamani yake ingeweza kumpatia kila Mtanzania gari aina ya Noah.

Rais Magufuli amefanya kazi kubwa kuweka ulinzi imara katika sekta hii ili iwanufaishe wananchi ikiwamo kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123 ili kuanzisha Tume ya Madini kwa lengo la kuleta ufanisi wa usimamizi wa sekta, kudhibiti utoroshwaji wa madini ghafi nje ya nchi na kuanzisha masoko ya madini.

Pamoja na kuongezeka kwa mapato kutoka mchango wa asilimia 3.4 mwaka 2015 mpaka 5.2 kwa pato la taifa, sekta hii imewapa fursa kubwa wachimbaji



wadogo kunufaika.

Kwa upande wa gesi, Bernard Membe na Kiongozi Mkuu wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, wanamtuhumu Rais Magufuli kushindwa kutekeleza ahadi yake ya kuzifanya Lindi na Mtwara kuwa kitovu cha uchumi wa gesi. Mradi unaozungumziwa ni wa dola za Kimarekani bilioni 30 (zaidi ya Sh. trilioni 60 za Tanzania), ambazo ni bajeti ya nchi kwa miaka miwili.

Tathmini inaonyesha kuwa, katika muktadha wa giliba na udanganyifu wa miradi ya rasilimali za nchi huko nyuma, ilikuwa busara ya hali ya juu kwa Rais Magufuli kusubiri na kutekeleza mradi katika muda muafaka kwa masilahi ya taifa. Mwalimu Julius Nyerere, mwasisi wa taifa la Tanzania, aliwahi kunukuliwa akitahadharisha kuwa rasilimali hizi haziozi, kwa hiyo hakuna sababu za kuharakisha kuingia mikataba isiyo na manufaa kwa taifa.

Nchini Msumbiji ambako miradi kama hii inatekelezwa, uzoefu unaonyesha kuwa tayari kuna migogoro inayoibua maswali ya kifisadi na hisia kuwa miradi husika haiwanufaishi wananchi. Zitto na Lissu, ambao wana historia ya kizalendo kupambania rasilimali za nchi, wanawachanganya wananchi wanapotaka mabeberu wapewe na kuvuna rasilimali hizi, badala ya kushukuru utulivu na tahadhari iliyochukuliwa ndipo washauri namna ambavyo rasilimali hizi zitawanufaisha Watanzania.

CHADEMA na ACT Wazalendo pia zimejenga hoja kuwa wakulima wa pamba (Mwanza) na korosho, mbaazi na ufuta (Lindi na Mtwara) hawanufaiki na mazao yao kutokana na biashara hodhi ya vyama vya ushirika. Wanasiasa hawa wanapigia chapuo soko huria ambalo kimsingi ni soko 'holela' kama vile "kangomba" au kwa kule Mbinga katika zao la kahawa wanaita 'magoma', ambao ni madalali wenye historia ya kuwanyonya wakulima.

Utafiti uliofanyika unaonyesha kwamba, mfumo wa stakabdhi ghalani na mauzo kupitia vyama vya ushirika, vina tija kubwa katika kumsaidia mkulima kunufaika na jasho lake.

Mfumo wa stakabadhi ghalani tangu uanze kutumika baada ya kupitishwa Sheria ya Bunge Na. 10 ya Mwaka 2005, umewezesha wakulima kupata bei za ushindani sokoni, kuongeza usimamizi na ubora wa mazao, umesisitiza matumizi ya vipimo rasmi, umejenga mfumo imara wa kitaasisi katika kusimamia mazao vikiwamo vyama vya ushirika. Pia umerahisisha ukusanyaji wa mapato ya serikali ikiwamo kodi, licha ya kuwapo kasoro ya kuchelewesha malipo kwa wakulima wakati fulani.

Hata hivyo, ushirika umewafanya wakulima kuunganisha nguvu na kuepuka hasara na unyonyaji unaofanywa na soko holela. Huenda kuna changamoto za kuboreshwa katika mfumo huu, ikiwamo kuviwezesha vyama vya ushirika kuwalipa wakulima malipo ya awali kwa wakati na kuwa na masoko ya uhakika.

Uchaguzi huu pia unashindanisha kiwango cha matarajio ya wagombea. Katika eneo la maono ya mbali ya kiuchumi, Rais Magufuli amewazidi washindani wake kwa kuleta uwiano wa utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati na uwekezaji katika huduma za jamii kitu ambacho hukioni katika ilani za vyama vya upinzani.

Uwekezaji wa miradi mikubwa kama reli, mradi wa kufua umeme wa Nyerere Mto Rufiji, upanuzi wa bandari, ujenzi wa meli na ujenzi wa barabara, ni miradi ya kimkakati yenye athari chanya katika uchumi. Miradi hii ambayo imeanza, inampa Rais Magufuli nguvu ya kuomba ridhaa ya Watanzania miaka mitano zaidi ili aimalizie.

Kwa umuhimu wa miradi hii ya kimkakati kwa uchumi, ingetosha kabisa Rais Magufuli awaombe Watanzania wafunge mikanda itekelezwe. Lakini bado yeye alileta uwiano akawekeza katika afya, elimu bure, usambazaji umeme vijijini kwa bei nafuu na kulipa madeni ya wafanyakazi. Maono haya ya kiuchumi, yanawashawishi wapigakura kupigia kura mwendelezo wa sera dhidi ya kuwapa wagombea wengine majaribio. Mnyukano wa mwingine kiajenda katika mtiririko huu ni ajenda ya uzalendo na utaifa. Wagombea urais wa ACT Wazalendo na CHADEMA wakikosoa msimamo wa Rais Magufuli kuwa hahudhurii mikutano ya kimataifa, hajajenga mtandao na viongozi wa mataifa makubwa nje ndiyo maana Tanzania haipati misaada kutoka kwa wafadhili.

Maswali ya kizalendo ya kujiuliza Watanzania ni kwa kiwango gani hawa viongozi wameelewa somo la kujitegemea kiuchumi? Je, wanadhani tu kuwa hao wanaoitwa wafadhili, ambao kimsingi ni mabeberu, wanamwaga pesa tu bure bila kujali masilahi yao?

Mwalimu Nyerere pia alishawahi kusema Watanzania wasitegemee kuwa kule nje kuna wajomba ambao watatoa pesa za bure. Katika agenda hii, Rais Magufuli anaonekana pia kupata vema, kwani ameiheshimisha Tanzania kwa kusimama na kutekeleza miradi mikubwa kama mradi wa umeme wa Mto Rufiji na miradi mingine kwa pesa za ndani.

Kwa wapigakura, hoja ya uzalendo bado ina mashiko zaidi kwamba Tanzania haiwezi kujenga uchumi imara kwa 'kujikomba' kwa wafadhili, ambao wanazitolea macho rasilimali za nchi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tumerejea, tunawaahidi wasomaji na wadau wetu

**BAADA** ya kuwa nje kwa miezi 18, hatimaye gazeti letu pendwa la Nipashe Jumapili limerejea rasmi huku likiwa na habari zilizofanyiwa uchunguzi wa kina, makala, burudani na michezo.

Katika kipindi chote hicho, wasomaji wetu walikosa uhondo waliokuwa wakiupata hatua ambayo ilisababisha wengi wao kuhoji kulikoni mpaka ukafikiwa uamuzi wa kulisimamisha gazeti hilo.

Pamoja na kuhoji huko, wengi walikuwa wakitoa ushauri wa kurejeshwa, hivyo kusikia maombi hayo na sasa tumerejea rasmi. Ni ukweli usiopingika kwamba wasomaji wetu walikosa mambo mengi ambayo yalikuwa yakiwapa burudani na elimu.

Kutokana na kusikia kilio cha wasomaji wetu na kuwa wasikivu, tunawaahidi kwamba tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu kuwaletea kile wanachokitaka kwa kuandika habari, makala na uchambuzi ili kutimiza lengo la kuelimisha, kuonya na kukosoa.

Pia tunaahidi kwamba tutaibua mambo ambayo yatasaidia kubadilisha mitazamo na mwelekeo wa jamii katika nyanja zote za kimaisha, yaani kisiasa, kijamii na kiuchumi. Lengo la hayo yote ni kuifanya jamii ya Watanzania kuwa na mtazamo chanya katika muktadha mzima wa maisha.

Katika kutekeleza hayo yote, tutazingatia weledi, taaluma na kujali matakwa ya kijamii na yale ya kisheria ili kuhakikisha mambo yote yanayoripotiwa katika gazeti hili yanafuata misingi ya kitaaluma na utawala wa sheria.


Wakati tukiahidi hayo yote, hatuna budi kuwakumbusha wasomaji wetu kwamba huo ndio wajibu wetu, kwa hiyo nao kwa upande wao wanapaswa kutumiza wajibu wao hasa kutoa ushirikiano unaostahili katika kutoa maoni yao. Kwa kufanya hivyo, ni dhahiri kwamba watatuwezesha kufikia lengo letu la kuhabarisha.

Pia wasomaji wetu, bila kujali taaluma zao, hawana budi kutoa maoni yao juu ya yale wanayoyahitaji kuwamo katika gazeti pamoja na kushauri yaliyomo ndani ili kuboresha habari zetu na kuwavutia wateja. Tunasema hivyo kwa sababu tunahitaji kuwa na ushirikiano mzuri baina yetu na wasomaji wetu.

Tunatoa rai pia kwa taasisi na mashirika ya umma na binafsi kushirikiana nasi katika kuuhabarisha umma kwa njia mbalimbali ikiwamo uhusiano chanya wa kibiashara. Imani yetu ni kwamba katika kufanya hivyo kutakuwa na mafanikio makubwa katika maendeleo ya nyanja husika na hatimaye kufikia malengo ya kitaasisi yaliyokusudiwa.

Kipekee, tunawaomba wasomaji na wadau wetu kutupokea na kushirikiana nasi katika kutekeleza jukumu letu la kuuhabarisha umma na kutoa elimu na mabadiliko ya jamii kwa ujumla katika nyanja zote za kimaisha.

Ni matumaini yetu kwamba ushirikiano chanya tutakaoupata kutoka pande zote utawezesha kufika katika upeo wa malengo tuliyojiwekea na hatimaye kutimiza kiu ya wadau wetu.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Uzoaji takataka mitaani ni kero kuliko uchafu wenyewe

Na Adam Fungamwango

**HIVI** sasa kila sehemu ina utaratibu wake kwenye masuala ya ulinzi na uzoaji takataka. Taratibu na kanuni hizo zinasimamiwa na serikali za mitaa kwenda kwenye kata na halmashauri nchini kote.

Kuna sehemu watoa huduma hizo kama vile takataka, wanatoza pesa kwa nyumba, huku wengine wakitoza kila chumba. Kuna watu wamekuwa wakipita kwenye makazi ya watu ukusanya fedha hizo kila mwezi.

Hii ni kwa sababu ya kuzuia wezi, lakini pia kuzuia utupaji holela wa taka ili kuzuia maambukizo ya magonjwa mbalimbali kama vile homa za matumbo na kipindupindu.

Jijiji Dar es Salaam, katika maeneo mbalimbali, kumekuwa na kero kubwa kuhusiana na uzoaji wa takataka, ambapo kumekuwa na ucheleshwaji mkubwa. Kuna wakati takataka zimekuwa zikionekana kukusanywa katika maeneo na kukaa hapo hata kwa wiki mbili kabla ya magari ya wazabuni wa kufanya kazi hiyo hayajafika kuzichukua.

Kinachofanyika ni kwamba wananchi hukusanya takataka kutoka kwenye makazi yao zikiwa ndani ya viroba na kuziweka maeneo waliyoelekezwa.

Hali hiyo imesababisha kero kubwa kwa sababu ya kukaa kwa muda mrefu kabla ya magari hayajafika , hivyo kuhatarisha afya za wakazi wa maeneo husika. Haijulikani ni kwa nini kumekuwa na ucheweshaji wa uzoaji, wakati wakazi hao wamekuwa wakitozwa pesa.

Kitachotakiwa kufanyika ni serikali za mitaa kupeleka pesa hizo kwa wenye magari ya kuzoa taka na kufanya kazi hiyo mara moja.

**Kuchelewa kwa magari kuzoa taka kwa baadhi ya maeneo yakiwamo Mwananyamala, Segerea na Tabata, kunaashiria kuwa kuna tatizo mahala. Je, pesa za kulipa malori ya takataka hazifiki kwa wakati? Kama siyo tatizo hasa ni nini? Ucheweshaji huo umekuwa ukisababisha matatizo mbalimbali mitaani.**

Kuchelewa kwa magari kuzoa taka kwa baadhi ya maeneo yakiwamo Mwananyamala, Segerea na Tabata, kunaashiria kuwa kuna tatizo mahala. Je, pesa za kulipa malori ya takataka hazifiki kwa wakati? Kama siyo tatizo hasa ni nini? Ucheweshaji huo umekuwa ukisababisha matatizo mbalimbali mitaani.

Kwanza kabisa, milima ya viroba ya takataka wakati mwingine unakuwa kando ya barabara, wakati mwingine kuzuia magari kupita hasa barabara zile za mitaani, hivyo kusababisha madereva kuteremka na kusogeza kwanza baadhi ya viroba ili kupita au kupishana.

Kero nyingine ni kwamba maeneo mengine ambako wanaelekezwa na serikali za mitaa ni kuweka nje ya nyumba za watu.

Baadhi wa wenye nyumba wa wapangaji wamekuwa wakilalamika hali hiyo kuwa inawafanya kulala kwa taabu kutokana na harufu ya takataka hizo kwani zinakaa muda mrefu bila kuchukuliwa na kusababisha funza kuanza kutoka kwenye viroba pindi mvua mvua zinaponyesha.

Hali hii inaondoa kabisa ile dhana ilivyojengwa mwanzo kuwa kuzoa taka ni kuleta usafi kwa jamii. Hali hiyo imekuwa kero kwani wakati mwingine inasababisha magonjwa ya kuambukiza.

Kuna baadhi ya wakazi wamekuwa wakidai kuwa kama kuna ucheleweshwaji wa kuzolewa takataka kwa sababu yoyote ile, basi takataka hizo zipelekwe na kuwekwa nje ya ofisi za serikali za mitaa, ili kama kutakuwa na ucheleweshaji, viongozi waone athari na huenda ikawafanya kukumbuka kusimamia magari kupita mitaani na kuchukua takataka kwa wakati.

Ni vyema serikali za mitaa zikachukua hatua kabla ya kusubiri mpaka magonjwa ya mlipuko yatokee ndipo hatua zichukuliwe. Ni bora kukinga kuliko kutibu.

## SAFU

### FIKRA MBADALA



Nkwazi Mhango, Canada

# Tunataka kampeni za kisasa si kisasi

KAMPENI kuelekea uchaguzi mkuu nchini zimeanza. Bila shaka, Watanzania, wanasiasa na wasio wanasiasa, wapiga na wapigiwa kura wako tayari kuushiriki kikamilifu kujipatia viongozi bora watakaowaletea maendeleo.

Kabla ya kuzama kwenye mada ya leo, tuwakumbushe wasomaji wetu wa siku nyingi: Tumerejea kwa kishindo baada ya miaka kama miwili ya kutokuwa hewani. Pia tunatoa salamu za rambirambi kwa taifa na familia ya rais mstaafu Benjamin William Mkapa aliyetutoka ghafla hapo tarehe 23 Julai, 2020 na kuzikwa kijijini kwake Lupaso, Masasi, Mtwara tarehe 30 Julai, 2020. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, Amina.

Tuingie kwenye mada yenyewe. Uchaguzi mkuu wa mwaka huu ni tofauti sana na chaguzi zote ambazo taifa letu limewahi kushiriki. Kwani:

Kwanza, uchaguzi unafanyika wakati dunia ikiendelea kupambana na janga la gonjwa la Covid-19 ambalo limesababisha madhira makubwa kwa mataifa karibu yote duniani. Pili uchaguzi mkuu unafanyika kwenye kipindi ambacho Tanzania imeshangaza wengi kuweza kuwa nchi ya uchumi wa kati kabla ya muda uliokadiriwa ukiachia mbali wakati mgumu wa janga la Covid-19. Tuchukue fursa hii kuwapongeza Watanzania wote kwa michango yao katika kufikia hatua hii adhimu na muhimu. Kwa upekee, tunaipongeza serikali ya awamu ya tano na Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho ni chama tawala na ambacho sera zake zimetuwezesha kufikia hatua hii kwa umahiri wao katika kusimamia uchumi hasa kipindi hiki kigumu baada ya kusimamiwa vizuri.

Pili, uchaguzi mkuu ni tukio kubwa na muhimu katika nchi ambapo wananchi hupata fursa kila baada ya miaka mitano kutumia na kufaidi haki yao ya kikatiba na kidemokrasia kuchagua viongozi wao watakaoongoza na kusimamia uendeshaji wa shughuli za kitaifa kwa miaka mitano ijayo. Hili si jambo dogo. Ni jambo linalohitaji maandalizi na utayari mkubwa kulishiriki na kulifanikisha kwa mustakabali wa taifa na watu wake.

Yafuatayo ni mambo muhimu tunayopaswa kuzingatia kama wananchi na wadau wa demokrasia na uendeshaji wa mambo yetu kama jamii, taifa na watu. Hivyo, lazima tuzingatie yafuatayo:

Mosi, kufanya kampeni na uchaguzi wa kistaarabu vitakavyohusisha sera na si matusi wala uzushi. Tunataka kampeni za kisasa na si za kisasi. Tunataka sera si shari. Tunajua; huu ni wakati wa kusema na kusikia mengi. Hata hivyo, mengi haya yatakayosemwa au kusikika yawe yana tija na si hadithi wala kelele za kupoteza fursa, muda na fedha za wananchi wanaogharimia zoezi hili adhimu na la bei mbaya kwa taifa. Hili ni muhimu; si kwa matokeo yanayokubalika na kukidhi haja bali kwa amani na usalama wa taifa. Kampeni za matusi na uzushi zipingwe na kupiga marufuku kwa nguvu zote ili kulinda tunu za taifa tulizorithi kwa waanzilishi wake. Kujenga amani ni sawa na kujenga nyumba. Ni vigumu kujenga nyumba, lakini rahisi kuibomoa. Gharama na muda wa kubomoa ni rahisi kuliko za kujenga.

Pili, katika uchaguzi mkuu, kama taifa tujiepushe matumizi mabaya ya uhuru wetu wa maoni kwa kujiepusha na kutishia amani na usalama wa taifa. Hivyo, hakuna haja ya kutishana wala kuminyana. Tujipe nafasi ya kunadi sera zetu na si matusi wala uzushi. Hakika tukifanya hivi, tutakuwa tumejihakikishia uchaguzi bora na mfano kwa wengine.

Kwani, ni wakati kama huu nchi nyingi huingia kwenye mtego wa maadui wa kuvuruga amani, utangamano na usalama wake bila kujua madhara yake. Tupingane kwa hoja na sera na si matusi na uzushi. Kwani, taifa litakuwapo baada ya kama ambavyo limekuwa kabla ya uchaguzi mkuu. Uchaguzi na wagombea huja na kupita. Lakini taifa litakuwapo siku zote.

Tatu, tuhakikishe haki inatendekea kwa wagombea wote. Wapewe nafasi sawa ya kunadi sera zao bila vikwazo wala vitisho ilimradi wote wazingatie sheria za uchaguzi na za nchi. Hivyo, katika kunadi sera, hakuna haja ya kusingiziana, kuzushiana, kuchukiana wala kudanganyana. Isitoshe ni ukweli usiopingika kuwa tutampata rais, wabunge na madiwani watakaokubaliwa na wale wanaotaka wawakilishe katika serikali yake. Pia wapo, tena wengi, ambao watashindwa. Kwani maana halisi ya uchaguzi, licha ya kuwa zoezi la kidemokrasia na kistaarabu, ni mchujo ambapo wengi huitwa na wachache huchukuliwa. Hivyo, kushinda na kushindwa ni matokeo halali ya uchaguzi ilimradi yafikiwe kihalali na kisheria.

Nne na mwisho, tujiepushe na vitendo vya rushwa na ulaghai na siasa rahisi rahisi za majitaka zenye kila dalili za takataka na uchakavu kulhali. Tufanye kampeni na siasa za uadilifu na uaminifu kwa ajili yetu na taifa letu kwa ujumla. Hapa lazima tuseme kuwa pande zote lazima kuwa makini kweli kweli katika matamshi na mipango yao. Wapiga kura nao lazima wapime sera, sifa na ahadi za wagombea wanaojitokeza mbele yao kuwashawishi. Maana wasipokuwa makini, watakuwa wamejitengenezea tatizo la miaka mitano ijayo.

**Kwa leo, tunaishia hapa. Tuonane wiki ijayo panapo majaaliwa.**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

# Binadamu bwana kwa meno pembe huwawezi!

KUNA mambo huwa yanaijia kichwani na hasa ninapokuwa nimekumbwa na mitafaruku ya kiuchumi na kuanza kukumbuka nilikotoka. Huwa na kumbuka kuwa miaka hiyo maisha yalikuwa muswano ile mbaya, kabla sijafulia leo.

Nakumbuka sana, hata kula haikuwa ishu kwa sababu chakula ndani kilikuwa chapwa na hata mashambani mambo hayakuwa mabaya, hivyo hakukuhitajika sijui fweza kwenda kununua chakula, kwa sababu tulikula na kusaza na ndiyo sababu ya kuwapo kiporo.

Tuliishi kama ndugu vijijini, tulipendana na kusaidiana, ingawa katika kila jamii hapakosekani wakorofi. Nakumbuka faza alikuwa kiongozi, nadhani kama si Mtemi basi Mwenyekiti wa Kijiji chetu.

Watu mara nyingi wakipita kumsalimia na wengine kumletea zawadi kwa heshima kubwa tu, nikazoea kuona wanawake wakipiga magoti, lakini nikishangaa hata wanaume wakimpigia magoti. Sikutaka kuuliza, unajua tu ni kwa nini.

Umwulize Mtemi kwa nini wanaume wanakuja kukupigia magoti kama wanawake? Unaweza kweli hata kama ni baba yako, si kuna mipaka, au mnanishauri vipi, ningemwuliza?

Ah! nikajiachia bora anaheshimika na sisi mikono inakwenda kinywani, misalani tunakuona, hivyo hakuna la kuharibika. Kwa hiyo, watoto wake na wadogo zake baba nao walionekana ni familia ya kifalme, hivyo kaheshima kidogo kalikuwapo au vipi?

Kuna watu waliokuwa wakionekana kuwa karibu saana na dingi, wakimsifia kwa sana, lakini sisi vitegemezi vyake na wadogo zake tukionekana kitimoto wenye mafua kwao.

Kila mara wakiwa klabu, utawasikia wakimsifu dingi kwa kila kitu na hasa katika masuala ya msingi ya kupambana na wanyama wanaovamia mashamba ya kijiji, lakini wakituona sisi walidai hatumsaidii chochote, sana sana tunamchafulia jina tu.

Walitusingizia kuwa sisi ni machokoraa tunajidai tumezaliwa na Mtemi, lakini tunamwaibisha kwa kuzurura ovyo na kuvuta bangi na kudai kuwa kama si sisi, pengine sifa ya Dingi ingevuka milima na mabonde, maziwa na mito, mabwawa na bahari na kufika ughaibuni, lakini tunamwangusha.

Ni hao hao waliokuwa wanaisifia familia hii ya kifalme, nasi tukiwamo, lakini utawasikia wakidai eti Dingi anafanya kazi sana, lakini sisi ni wa kuchoma tu kama wezi.

Tukawa tunayasikia haya, tunabaki kusikitika tu kwa kuwa hata hiyo bangi sisi hatukuwahi kuiona.

Tukawa tunawashangaa wanaoisifia familia ya kifalme, lakini inabagua watoto wa mfalme, wake zake na wadogo zake? Unaisifia familia vipi, huku unang'ang'ania kwa baba yetu na sisi unatuona si mali kitu, wakati unajua kabisa ukisema familia, nasi tumo na ukisema familia, ujue unazungumzia damu yetu!

Mara nyingine walikuwa wakija kumwona Dingi na kila walichokisema kujisifia, aliwaangalia na kutikisa kichwa na kisha akacheka, kwa sababu aliwajua jamaa hawa wanachokitaka kwake ni kujikomba tu, ili siku moja asije akachacha na kuwaambia matarishi wetu wawashughulikie.

Kwa kuwa sisi mara nyingi tulijichanganya na watoto wenzetu wa kijijini, bila kujali uwezo wa wazazi wao, tulisikia mengi kutoka kwa watoto hao, wakituambia jinsi wazazi wao wanavyomsema Dingi kifichoni, lakini wakimchekea hadharani-jino pembe hilo, tena lile la ngiri.

Unaweza kukutana na ngiri ukadhani anakuchekea, kumbe kashindwa tu kuficha jino lake, kutokana na urefu wake na kumbe kanuna ile mbaya na akitamani akumalize.

Binadamu nao wako hivyo, unamwona anatabasamu, lakini kumbe mawazo yako mbaali. Ukitaka kujua na kuthibitisha waulize wanakwaya.

Sisi zamani tukiwa shule hizo za chandimu, tukiwa katika kwaya ya shule, mwalimu wetu wa kwaya, namkumbuka kwa jina moja la Kumbo, kama yupo Mungu aendelee kumlinda na kama alishatangulia basi aendelee kulala hapo pema, nasi twaja atuwekee matandiko.

Yeye katika mafunzo yake, mbali na a e i o u ya uimbaji...doremifasolatido...alikuwa akitukumbusha kuwa kila mwanakwaya anapaswa kutabasamu, hata kama atakuwa hajala, siku hiyo atakayokuwa mbele ya kiongozi au katika mashindano ya kwaya.

Kwamba hata kama wakati mnaimba, bahati mbaya mwenzenu mmoja asiye na akili nzuri au bahati mbaya alifakamia mandondo yaliyolala, amejikuta anachafua hewa miongoni mwenu, wala msishituke na kuguna, bali hapo sasa ndipo linahitajika tabasamu pana zaidi na kunyonga maungo kwa bidii.

Akawa anatwambia kuimba wimbo mmoja kunahitaji kuvumilia kwa muda fulani tu na hata kuonyesha meno yako hadharani, hakupunguzi chochote na wala si gharama kubwa. Ni kukenua tu huku ukiimba, ili msikilizaji au jaji aone kweli kwaya mnaiweza. Binadamu usiwaamini sana.

**Simu:+255 713410008 na baruapepe:jkulangwa@yahoo.com**

## KONA YA UKWELI

# Vyama visitumie wafuasi kuvunja amani



Na Thobias Mwanakatwe

UCHAGUZI wa viongozi katika nchi ni utaratibu rasmi unaoendeshwa kwa mujibu wa sheria. Kupitia uchaguzi, wananchi wanawezeshwa kufanya uamuzi wa kupata viongozi kwa njia ya demokrasia.

Nchini Tanzania, uchaguzi wa madiwani, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge na Rais hufanyika kila baada ya miaka mitano. Kupitia uchaguzi huo, wananchi hutumia fursa hiyo kuchagua viongozi wanaowaona watawaletea maendeleo katika maeneo yao.

Uchaguzi huo huratibiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ambazo huratibu shughuli zote za uchaguzi kwa lengo la kuufanya uwe huru na wa haki.

Mwaka huu Watanzania wanafanya uchaguzi kuwapata viongozi na sasa mchakato uko katika hatua ya kampeni. Vyama mbalimbali vimeweka wagombea na vinafanya mikutano ya kampeni kunadi sera zao kushawishi wananchi wawachague.

Oktoba 28 ndiyo siku maalum kwa Watanzania kupiga kura kuchagua viongozi watakaowaongoza kwa miaka mitano ijayo. Huu utakuwa uchaguzi wa sita toka nchi ilipoingia katika mfumo wa vyama vya siasa mwaka 1992.

Wakati kampeni zikiendelea, tumeanza kushuhudia katika baadhi ya maeneo kukitokea vurugu na baadhi ya wagombea kutumia maneno makali yanayohatarisha uvunjifu wa amani.

Mfano katika mjini wa Tunduma mkoani Songwe, kulitokea vurugu katika Kata ya Majengo kati ya wanaodaiwa kuwa wafuasi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kusababisha mtu mmoja kufariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa.

Sote tunafahamu kuwa amani katika Tanzania ni tunu kwa Watanzania wote. Kila mmoja amechangia kuilinda na kuidumisha. Hakuna aliye na hakimiliki ya amani ya nchi hii.

Kauli za uchochezi ambazo bahati mbaya zinatolewa na baadhi ya wagombea wa urais zinawajaza hasira na kiburi wafuasi wa vyama vyao ambao nao bila kufanya utafiti, wanaona maneno wanayoelezwa kama yana ukweli au la.

Wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi mwaka huu lazima watambue kuwa kukitokea vurugu nchini nao hawatasalimika kwa hiyo ni wakati mwafaka wa kuangalia wazungumze nini na kwa wakati gani kwenye mikutano yao ya kampeni.

Ni lazima tujifunze kutoka nchi kadhaa za Afrika ambazo zimeingia kwenye machafuko, chanzo kikiwa wanasiasa kuhamasisha vurugu kwa wafuasi wao kutokana na kujazwa vichwani mwao mambo yasiyo ya msingi na afya kwa nchi.

Tunawaomba wanasiasa watambue kuwa amani ni muhimu sana kuliko siasa zao na kuna maisha baada ya uchaguzi. Tusiitumbukize nchi yetu kwenye machafuko halafu na nyie waanzilishi mkakimbia na kutuacha kwenye matatizo.

## DARASA LA NDOA

# Ni haki ndugu, wakwe kuingilia ndoa?



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0655865555

WATU wengi wanatamani kuoa au kuolewa. Ni jambo jema kwani Mungu alianzisha taasisi ya ndoa ili watu waitamani, waingie na kuifurahia.

Hata hivyo, watu wengi wameivamia taasisi hii pasipo kujua unyeti, maana na misingi yake. Wako wanaofikiri kuwa ndoa ni jambo la kawaida na kwamba baada ya kuoa au kuolewa, furaha na starehe zinakuja zenyewe bila kutengenezewa mazingira.

Vijana wengi hawaandaliwi vya kutosha kabla ya ndoa, hivyo kusababisha kuingia katika taasisi hii wakiwa na ufahamu mdogo kuhusu ndoa. Kwa bahati mbaya sana, jitahada kubwa zimewekwa katika kuandaa sherehe kubwa za arusi na si kuwandaa vijana kuwa waume na wake bora. Matokeo yake ni ndoa kutokudumu.

Ndoa ni taasisi ya kijamii iliyo huru na inayojitegemea. Aidha, ndoa ni mabadiliko ya mtu kutoka katika hali ya upweke na kuwa mke au mume wa mtu. Badiliko kubwa la pili, ni la kiuhusiano kati ya wazazi na watoto wanaooa au kuolewa. Tangu siku ya harusi, uhusiano wa mwanaume au mwanamke na wazazi wake unapunguzwa na uhusiano mkubwa unakuwa na mke au mume wake.

Mwanaume anapooa au mwanamke anapoolewa, uhusiano wake na mwenzi wake ni jambo la msingi na kipaumbele cha kwanza. Kwa msingi huo, vijana wanapoandaliwa kuingia katika maisha ya ndoa wanahitaji kuandaliwa kisaikolojia kukabili mabadiliko haya, kuacha mazoea. Pia wazazi na ndugu wanahitaji kufahamu mabadiliko haya ni muhimu kwani mambo hayatakuwa kama yalivyozoeleka hapo awali.

Vijana wanapaswa kuandaliwa kuondoka, kujitegemea na kuwa na uhuru wa kuendesha maisha yao ya ndoa bila kuingiliwa wala kushinikizwa. Kuishi kwa mashinikizo na kuongozwa na watu wengine ni dalili ya kutokukua kwa wanandoa. Hali hii huondoa uhuru na kujiamini kwa wanandoa katika kuendesha na kusimamia maisha yao ya ndoa.

Katika badiliko hili kubwa, kunajengwa familia mpya. Wanandoa wanahitaji kujenga utambulisho wao, hivyo kujitenga kwa kiasi fulani, kutoka kwa wazazi na ndugu zao kimwili, kihisia, kiufahamu, kimaamuzi na kimapato.

Wanandoa hao wanapaswa kuwa na uhuru na faragha binafsi; uhuru katika kufikiri mambo yenye faida ya ndoa yao; uhuru katika kufanya uamuzi wa mambo mbalimbali yanayohusu maisha yao na wazazi wao au ndugu zao; uhuru katika mapato na matumizi kwa ustawi wa familia yao. Wanandoa wanakuwa na mamlaka na utawala kamili.

Mtu akiwa ameoa au kuolewa maana yake amekua mtu mzima mwenye uwezo wa kufanya uamuzi, hivyo mwanandoa kusubiri kuambiwa afanye nini au kufuata kila kitu wazazi au ndugu wanachotaka au wasichotaka, ni kuikosea ndoa na matokeo yake ni misuguano na ugomvi ndani ya ndoa. Nafasi ya mwenzi inakuwa haipo tena.

Wazazi au ndugu hawana tofauti na watu wengine wowote kwenye jamii au duniani. Kuwa mzazi haina maana ya mtu kuwa na thamani zaidi ya mwingine. Sifa ya awali ya kila binadamu ni ubinadamu wake. Sifa za ubaba, u-mama, u-dada au u-kaka ni utambulisho wa kijamii.

Baba au mama, kaka au dada wanastahili kuheshimiwa kama binadamu kwanza, halafu kama ndugu au wazazi. Kuwa ndugu au wazazi hakuwapi haki wala uwezo wa kuingilia ndoa za watoto wao au ndugu zao. Pamoja kwamba mtoto hakui kwa mzazi, inapofikia hatua ya ndoa, kuna mipaka ya kutunzwa na kuheshimiwa na wazazi ili ndoa ikue. Kukua huko ni pamoja na kujua kwamba hata mzazi anaweza kukosea kama binadamu mwingine yoyote.

Kuoa au kuolewa hakumaanishi kutelekeza au kuondoa nafasi ya wazazi kwa watoto bali kutoa uhuru kwa watoto waliooana kuendesha maisha yao ya ndoa bila kuingiliwa wala kupokea amri kutoka kwa wazazi.

Kufanya hivyo ni sehemu ya kuheshimu mipaka ya ndoa na kutambua kuwa sasa watoto wao ni watu wazima wenye uwezo wa kufanya maamuzi na wenye majukumu mapya.

Wazazi wanaweza kutoa ushauri pale unapohitajika na lakini si kutoa amri au mashinikizo. Aidha, Wazazi wanatazamiwa kutoa ushauri wenye kujenga na kuimarisha ndoa ya watoto wao badala ya kuwavuruga na kuwagawa.

Kuna wazazi ambao hawako tayari kukubali kuwa mamlaka yao kwa watoto si ya milele, kwani upo wakati mamlaka hayo yanakuwa na mipaka. Kuna hatua katika maisha ni lazima mtoto atakuwa na haki ya kuamua juu ya maisha yake, hivyo wazazi wanapokuwa waamuzi wa kila jambo linalowahusu watoto wao pale wanapokuwa wameoa au kuolewa, kusababisha migogoro katika ndoa za watoto wao.

Wazazi wengine wamekuwa waamuzi wa maisha ya watoto wao katika ndoa. Mzazi anaweza hata kumpangia mwanawe ampe fedha kiasi fulani kila mwezi kwa sababu tu yeye ni mzazi. Mzazi anaweza kumpangia mtoto aishi vipi na mkewe au mumewe, awalee vipi watoto wake na masuala mengine ya kimaisha. Katika hilo wanasababisha watoto wao kwenye ndoa kushindwa kukua.

Wanandoa wasioruhusiwa kukua, huwa hawako tayari kwenda kinyume cha utashi wa wazazi au ndugu, hata kama wanauona utashi huo ni kinyume cha matakwa yao.

Ndoa ni ushirika na kuinuana ili kufikia malengo, hivyo, wanandoa wanahitaji kuishi katika ushirika kwani ni watu wanaotegemeana. Mwenzi anakuwa sehemu ya nafsi ya mwenzake. Ni watu walioungana kiroho, kiakili, kimwili, kihisia, kimapato, na mambo mengine. Mke anatimiliza kilichopungua kwa mumewe, kama jinsi sifa za mke zinavyokamilisha zile za mume. Kila mmoja anakuwa sehemu ya mwenzake na wanaendesha maisha yao kwa umoja.

Kabla ya ndoa kila mmoja alikuwa akifikiri na kutenda binafsi. Lakini baada ya kuoana, mambo yote, ikiwa ni pamoja na yale yanayohusu kutoa misaada kwa wazazi, ndugu na watu wengine, yanapaswa kufanywa kwa kushirikiana, kushauriana na kukubaliana.

Kufanikiwa katika ndoa juhudi ya wanandoa wote wawili inahitajika. Ni lazima wote wawili watamani na kutaka ndoa ikue na kuwa yenye furaha. Kila mmoja katika ndoa ni lazima ajitahidi kwa bidii zake zote, hali akishirikiana vyema na mwenzi wake katika kukabiliana na changamoto zote katika ndoa na kujitahidi kuufanya uhusiano wao kuwa mwema zaidi.

# MAISHA

SEPTEMBA 6, 2020

Nipashe


Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




## HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 10

**Watoto wakijibiwa kitoto, akili zinadumaa**



## MAISHA NI NYUMBA

Unataka kujenga? Anza namna hii

Ukurasa 15



**Sandwich za nyama ya ham na parachichi**

Ukurasa 14



KUWA NA NGOZI LAINI

# Maajabu ya matunda mwilini

Ukurasa 14

# Watoto wakijibiwa kitoto, akili zinadumaa

MACHOZI mepesi yalinitiririka juu ya mashavu yangu baada ya kupiga mwayo, yalifanya mtoto aliye karibu nami aniulize: "'Unalia' nini?" Akimaanisha ninalizwa na nini?

Nilimwangalia, kisha nilitabasamu, halafu nikamjibu kuwa machozi yangu yalitokana na mwayo. Mtu akipiga mwayo, wakati mwingine machozi humtoka.

Yule mtoto hakunielewa, akaniuliza tena, "Mwayo ndio nini?"

Nilimwangalia tena, lakini sikuwa na jibu jepesi la kuitosheleza akili yake ya kitoto. Nikaona nikianza kumfafanulia kisayansi mwayo ni nini, kwa umri wake wa miaka mitatu au minne hivi, hawezi kunielewa.

Kwa hiyo nikamjibu kivivu, "Mtu akichoka, anapiga mwayo. Anafumbua mdomo, halafu anafanya hivi (nikawa namuonyesha mfano wa mtu akipiga mwayo)."

Akaacha kuniangalia usoni, huku akiendelea na michezo yake, akaniambia; "Mi baba yangu akichoka analala tu, halii (hapigi mwayo)."

Nikacheka, bado katika akili yake aliona kile nilichofanya ni kulia tu, lakini ila kuendeleza maongezi yetu na



kutaka kujua kama na yeye anapiga mwayo, nikamuuliza: "Wewe 'unaliaga'?"

Akatulia kidogo, akaacha kucheza na kuniangalia, Akaniambia: "Mi silii, ila nililia wakati Junior alipochuka gari langu nikalia. Wewe unamjua Junior?"

Kabla sijamjibu swali lake, akaja rafiki yangu, akaniambia: "Yani jinsi unavyoongea na huyu dogo unaonekana kama unaongea na mtu mzima." Nkamuuliza; "kwa nini?" Akaniambia: "Nilikuwa nakuangalia muda mrefu, mnaonekana kama watu wazima wawili mna maongezi ya maana sana."

Hili ndilo tatizo kwa baadhi ya watu wazima wengi ambao wanaamini kuwa watoto wadogo hawana mambo ya maana ya kuzungumza au kuongea na watu wazima. Wanaamini watoto ni watu kwa kukaa nao na kuzungumza nao mambo ya kitoto tu.

Kutokana na mazoea kuwaona watoto wanapaswa kujibiwa kitoto, makuzi yao nayo yanabaki kuwa ya kitoto toto. Kutokana na mazoea hayo hata umri wa mtoto utakapozidi hawezi kuongeza uwezo wake wa kupambanua mambo kwa sababu tu hakupewa nafasi ya kuongozwa katika hilo.


Uwezo wa kiakili wa mtu ye yote unajengwa kwa kupata maswali yanayomzunguuka kichwani mwake na kwa mtoto mdogo njia pekee ya kupata majibu ya maswali yake ni kupata majibu kutoka kwa watu wazima wanaowaamini. Tuwasaidie.

## NA KHAMIS KIDAGO

0657 207168

## QUIZ

1. Jaza nafasi zilizokuwa wazi kuhusu vifaa vya darasani kwa lugha ya Kifaransa.



Les objets de la salle de classe

Instructions: Fill in the blanks with the name of the objects below. Use the word bank at the bottom of the page to help you!

1. ______ 2. ______ 3. ______
4. ______ 5. ______ 6. ______
7. ______ 8. ______ 9. ______

| | | |
|---|---|---|
| des ciseaux | une gomme | un feutre |
| un crayon | un livre | de la colle |
| un stylo | un cahier | une règle |

2. Unajua majina ya sehemu za mwili wa binadamu kwa lugha ya Kifaransa? Taja sehemu hizi kwenye mchoro.




3. Siku zifuatazo ziko kwa Kifaransa, andika maana yake kwa Kiswahili. N:B siku kwa kifaransa huandikwa kwa herufi ndogo.

- lundi........................
- mardi........................
- mercredi...................
- jeudi.........................
- vendredi...................
- samedi.....................
- dimanche..................

4. Andika miezi yote kwa Kifaransa. (Januari mpaka Desemba)

N:B miezi yote, kwa lugha ya kifaransa, huandikwa kwa herufi ndogo.

- ¬ ....................................
- ¬ ...........................
- ¬ ....................................
- ¬ ...........................
- ¬ ...........................
- ¬ ........................
- ¬ ...........................
- ¬ ...........................
- ¬ ...........................
- ¬ ...........................
- ¬ ...........................
- ¬ ...........................

5. Andika namba zifuatazo kwa tarakimu.


Mfano: zéro – 0

- Un.............
- Deux...........
- Trois...........
- Quatre.........
- Cinq...........
- Six.............
- Sept...........
- Huit...........
- Neuf...........
- Dix.............
- Onze.......................
- Douze.......................
- Treize.......................
- Quatorze....................
- Quinze.......................
- Seize..........................
- Dix – sept....................
- Dix – huit....................
- Dix – neuf....................
- Vingt...........................
- Vingt-et un....................
- Vingt-deux.....................
- Vingt-trois.....................
- Vingt-quatre...........................
- Vingt-cinq.............................
- Vingt-six...............................
- Vingt-sept..............................
- Vingt-huit..............................
- Vingt-neuf..............................
- Trente......................................


***Majibu ya maswali haya yatatolewa Jumapili ijayo**

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO



A lichokifanya daktari

Doktari mmoja alikwenda kula na kumuacha msaidizi wake aendelee kutibu wagonjwa.

Aliporudi alianza kumhoji msaidizi wake

Doktari: uliwaona wagonjwa wangapi?

Msaidizi: " Nliwashughulikia wagonjwa watatu, mmoja aliumwa kichwa nikampa panadol"

Doktari: "Safi sana, na wa pili?"

Msaidizi: "Wa pili alikuwa anaumwa na tumbo, nikampa flagyl"

Dokta: " safi sana, na watatu je?

Msaidizi: Alikuja mtu amevurugikiwa akili, nikampa dawa ya matone ya macho"

Dokta: "Tobaaaa?"

==================

**SWALI**

Mnyama mwenye shingo ndefu anaitwaje?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kila ninayempata siyo mke wangu, balaa gani hili?

MPENZI msomaji, karibu tena katika safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Safu hii imerudi tena kukonga nyoyo za wasomaji wake baada ya kutokuwapo kwa kitambo sasa ndani ya gazeti hili linalopendwa na wengi.

Yupo msomaji mzuri wa safu hii aliyejitambulisha kwa jina moja, Jeremia, mwenyeji wa Mkoa wa Kigoma. Hivi majuzi aliwasiliana nami kutaka kuweka bayana yanayomkuta baada ya kuvumilia kwa miaka kadhaa.

Kupitia ujumbe wake mfupi kwenye simu ya kiganjani akasema hivi; "Anti, nina tatizo ambalo naamini utanisaidia hata kwa ushauri tu. Nina mke wangu sasa ni mwaka wa nne amekataa kurudi nyumbani, nifanyeje?

Baada ya ujumbe huo ilibidi nimpigie simu jamaa huyu ili niweze kujua mazingira anayopitia katika ndoa hii. Niliweza kumuuliza maswali kadhaa, ikiwa ni pamoja na kujua mahali alipo kwa sasa, na mkewe huyo naye yuko wapi na ilikuwaje kila mmoja akawa mbali na mwenzake.

Akafunguka na kusema hivi;-

Mimi na mke wangu ni wenyeji wa Kigoma. Tulioana huko Kigoma. Mwaka 2014 nikahitajika Mwanza kwenda kuhubiri injili. Ikabidi mimi na mke wangu tuondoke kwenda Mwanza.

Hata hivyo, tangu tuwe huko Mwanza, uhusiano haukuwa mzuri kwani kila wakati ilikuwa ni mizozo isiyoisha ndani ya ndoa. Mke wangu akawa kama hanitaki, kila ninachomwambia ananipinga kama vile siyo mke wangu.

Nilipoona mambo yanakuwa magumu nikaamua kundoka kurudi kwetu Kigoma. Nikamwambia tuondoke wote, yeye akakataa. Nikaondoka na kila nilipowasiliana naye kumwambia arudi nyumbani akawa ananijibu 'hajisikii kurudi', nikitaka nimfuate. Ni mwaka wa nne sasa amegoma kurudi Kigoma.

Msomaji wangu, baada ya maelezo hayo, nikamuuliza, je, baada ya msimamo huo wa mkewe, bado anampenda? Na kwamba, je, anadhani bado anapendwa? Au, je, anahisi pengine mkewe anaye mtu mwingine anayemzuzua huko Mwanza ndio maana hataki kurudi Kigoma?

Ndugu huyu akasema: "Mimi bado nampenda ila sijui kwanini ananikataa. Pia nadhani hana mtu kwa kuwa pale nilipomuacha bado yupo, na nikiongea na majirani wanasema yupo peke yake. Ila pale jirani yupo jamaa mmoja ambaye alikuwa akimkodolea sana macho mke wangu, sasa sijui kama anaweza kuwa chanzo cha mama kugoma kurudi kwetu.

Ndipo nikamuuliza tena jamaa sasa ana uamuzi gani kwa upweke huu, akajibu, 'Baada ya mke wangu kunikatisha tamaa, hapa Kigoma niliamua kutafuta mwanamke mwingine nikampata binti mmoja tukaelewana nikawa nampatia zawadi mbalimbali.

Akanitambulisha pia kwa wazazi wake. Moyo ukatulia.

Baada ya miezi takriban sita mama yake binti huyu akaniuliza. Je, umempenda binti yangu? Nikamwambia ndiyo. Akasema, "Binti alikuwa ameolewa, na mume wake yuko Morogoro kwa shughuli za biashara".

Nilibakia mdomo wazi sikujua cha kufanya. Ilibidi niachane na familia hiyo. Nikawa nawaza, je, mbona kila ninayempata siyo mke wangu? Wa kwanza kanikataa, na huyu naye kumbe ni mke wa mtu. Nikawa njia panda.

Wakati natafakari, nikawasiliana na rafiki yangu anayeishi Iringa nikamsimulia yanayonikuta, akaniambia atanichunguzia mwingine pale Iringa. Akampata dada mmoja ambaye alikuwa ameolewa na mumewe akafariki baada ya kuangukiwa na kifusi machimboni. Alikuwa amezaa naye mtoto mmoja. Akanipa namba tukawasiliana na hivi sasa niko mbioni kwenda Iringa kuonana naye." Anamaliza kisa chake kijana Jeremia.

Mpenzi msomaji, Bila shaka umepata picha naisha ya kijana huyu. Hapa zipo roho mbili zilizosimama mbele ya Jeremia. Kwanza ni roho ya kukataliwa. Roho hii humfanya mtu asikubalike mbele za watu.

Ni silaha ambayo ibilisi huitumia kuharibu hatma ya mtu na kuweka ukuta ili ashindwe kuunganishwa na watu waliobeba Baraka zao.

Pili, ipo roho ya mitala inayomtesa yeye pamoja na wanawake anaokutana nao. Roho ya mitala husababisha ndoa za wake wengi, kuolewa na wanaume wengi, kuoa na kuacha, kuolewa na kuachika. Pia husababisha kukosekana kwa upendo kati ya wanandoa, kutokufurahia ndoa, ugomvi usioisha, inasababisha hatma za watu wengi kuharibika.

Kadhalika, ni chanzo cha ndoa nyingi kuharibika, na kuwafanya watu wawe wajane katika umri mdogo. Maisha Ndivyo Yalivyo. Tukutane tena wiki ijayo.

Je, una maoni au ushauri wowote kwa jamaa huyu? Tuma ujumbe mfupi kupitia simu ya kiganjani, 0715268581 ambayo pia ipo kwenye WhatSapp.

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Matusi, udhalilishaji majukwaa ya siasa hayafai

KIPENGA cha uchaguzi mkuu 2020 kimepulizwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na sasa wagombea wa ngazi za urais, ubunge na udiwani wameanza kunadi sera zao katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Kampeni hizo ambazo kwa sasa zimeshika kasi katika nafasi za urais kwa wagombea kufanya mikutano ya kuomba kura za wananchi wa mikoa mbalimbali, lengo ni kuomba nafasi ya kuliongoza taifa kwa miaka mitano ijayo.

Tayari nyenzo za kufanya uchaguzi huo zimetolewa ambazo ni Sheria ya Uchaguzi, Maadili na kanuni ambazo zimeeleza wajibu wa kila mshiriki wa uchaguzi mkuu, katika kuhakikisha siku 64 zinamalizika salama na nchi inapata viongozi wa ngazi hizo kwa amani.

Nyenzo zilizotolewa ni mwongozo tosha kwa kila mgombea na wadau wote kuhakikisha kampeni zinakuwa za amani, na wananchi wanapata nafasi ya kufanya maamuzi sahihi katika sanduku la kura.

Katika baadhi ya maeneo ambayo kampeni zimeanza, kumejitokeza lugha zisizo na staha, zenye kudhalilisha jinsi na jinsia, kwa lengo la kumdhoofisha mgombea mwingine au chama anachotoka, jambo ambalo halipawi.

Kwenye mitandao ya kijamii imesambaa video ya mgombea ubunge mmoja akinadiwa na kiongozi mmoja, lakini badala ya kunadi sera, moja kwa moja alimshambulia mgombea mwingine wa jinsia tofauti, hali ambayo imeleta ukakasi.

Kwa kipindi hiki ni lazima kuwe na uwanja sawa wa kucheza mpira, na watazamaji kupata nafasi ya kuangalia mpira husika kisha kutoa alama kwa mchezaji wanayeona anastahili kushinda.

Vyama vina vyenzo zao ambazo ni ilani ya miaka mitano ambazo wanazinadi kwa wananchi, ikiwa atapata ridhaa ya kuongoza miaka mitano ijayo watafanya nini katika kila sekta inayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja.

Wananchi wana kiu ya kusikia Ilani za vyama ili ziwaongoze kufanya uamuzi sahihi, bila kuwafafanulia vyema watashindwa kufanya uamuzi ambao unaamua maisha yao kwa miaka mitano ijayo.

Haipendezi na haikubaliki kumtukana au kumdhoofisha mgombea mwingine kwa lengo la kupata umaarufu au ushindi, bali kunadi sera ambazo zitawauza na kuwatambulisha kwa wananchi ili waamue nani atafaa kuwa rais, mbunge na diwani wao.

Vyama vihakikishe vinasambaza ilani zao katika nyaraka ndogo ndogo na rahisi wananchi kusoma na si vitabu vikubwa ambavyo kwa namna moja au nyingine wananchi ambao hawana utamaduni wa kusoma watashindwa kufanya hivyo.

Vyama vihakikishe vinawafikia wananchi hadi ngazi ya kitongoji, na visitumie kutokujua au kuelewa kwao kuwarubuni kwa zawadi au fedha ili wakubalike na kuingia kwenye nafasi.

Wananchi wasikubali kupokea maneno matupu, wasome nyaraka, yaani Ilani za vyama ambazo ndiyo mwongozo, ili wanapotoa kura kwa mtu fulani inakuwa ni baada ya kumsikiliza na kulinganisha na alichoandika katika ilani.

Katika kipindi hiki kupitia kiungo kidogo ambacho ni ulimi taifa linaweza kuparaganyika na kulirudisha kwenye mstari ikawa ngumu sana.

Zipo nchi nyingi za Afrika ambazo ziliingia kwenye vita ya wenyewe kwa wenyewe, machafuko ambayo yalichukua muda mrefu kurejesha hali ya amani na utulivu nchini.

Kutaja kwa uchache, Kenya iliingia kwenye machafuko mwaka 2008, Somalia, Burundi, sababu kubwa ikiwa ni kutanga kuingia Ikulu kuongoza taifa, lakini kutawaliwa kwa lugha za kuligawa taifa na chuki zilipandikizwa kwenye mioyo ya wananchi.

Chuki ndani ya mioyo ya watu haipandikizwi siku moja bali kidogo kidogo na wishowe nguvu ya umma inapoamua hata mtutu wa bunduki hauwezi kuzuia, hivyo ni lazima kuziba mianya inayoonekana kwa sasa ikiwa ni dakika za awali kabisa za kampeni.

Wanasiasa wanapokuwa katika majukwaa ya kisiasa wanadi sera zao na si maneno ya kuwagawa watu kulingana na ukanda, itikadi, makabila, rangi zao na inapofikia hapo maana yake wagombea wamefilisika kisera hawana cha kueleza umma.

Tanzania imesifika na kutegemewa na nchi nyingine kwa kuwa taifa la mfano lenye umoja ambao ulijengwa na Baba wa Taifa kuhakikisha tuna taifa moja lisilo na ubaguzi wa dini wala kabila, kiasi cha kuoa na kuolewa bila kuuliza kabila la mtu.

Jambo hili lisiingie dosari sasa kwa siasa za majitaka, za kugawa watu kulingana na ukanda wanaotoka, dini wanayoamini au rangi zao, ikiwa hivyo ni kuteketeza taifa au sawa na kuendelea kujenga mambo wa chuki mioyoni mwa watu, na kuwafikisha pabaya.

Wanasiasa wahubiri amani siku zote, wahubiri misingi ya taifa pasipo kuwagawa watu vipande vipande.

# HARUSI









Ilikuwa ni harusi ya kufana kati ya Injinia Johnson Semizigi na Injinia Mecktrida Ruteza, iliyofungwa katika Kanisa la Mtakatifu Albano Upanga, Agosti 29, 2020 jijini Dar es Salaam na baadaye kufuatiwa na sherehe bomba katika ukumbi wa Sapphire, Mbezi Beach.

## Johnson & Mecktrida

MITINDO

# 'MARIDAAD'

# Inapendeza zaidi ukivaa Sweetpants na Timberland




DUNIA ya mitindo ina uwanja mpana, licha ya kutofautiana aina gani ya mitindo ya mavazi inayopendwa, watu wote wanaona umuhimu wa kwenda pamoja.

Uvaaji si lazima kufuata makundi au wanachopenda kuvaa wengine, jambo zuri ni kuangalia aina ya vazi ambalo linaweza kukupa umaridadi na tabasamu pana.

Viatu vya aina ya Timberland, ni chaguo zuri kutokana na kutochuja katika muonekano wake na hutumika nyakati zote katika mwaka.

Aina hii ya viatu vya buti vilianza kuvaliwa nchini Marekani mwaka 1918, kama vazi la kazi hasa katika viwanda vya mbao. Hata hivyo ubora na muonekano wake vilipendwa na watu wengi na kusambaa duniani kote.

Shukrani zote zinakwenda kwa mbunifu wa kwanza Nathan Schwartz, ambaye alivumbua kiatu hicho kwa nia ya kuwakinga wafanyakazi, lakini hakujua kama vitakuwa lulu kwa vijana na wanaume wa nyakati zote.


Leo watu wote wanaume na wanawake wanavaa viatu hivyo, huku wakichagua matoleo maarufu kama vile classic ya njano, 'simpo' viatu vyepesi, buti, sneakers na moccasins.

Aina hii ya viatu unaweza kuchagua rangi kulingana na wewe unavyopenda, unaweza kuvaa vya rangi ya njano, dhahabu, machungwa, nyekundu, kijivu, nyeusi, nyeupe, kahawia, nyeusi na bluu. Viatu vya aina hii inapendeza zaidi ukivalia na suruali ya jeans, kaptula za aina zote, fulana au shati, mavazi ya michezo au sweatpants.



URBEMBO

# KUWA NA NGOZI LAINI
# Maajabu ya matunda mwilini



UREMBO ni suala lisiloepukika katika maisha ya kawaida ya mwanamke. Katika kuweka muonekano wa kuvutia, ni lazima kuzingatia njia mbalimbali ikiwamo ulaji, unywaji, mazoezi na matumizi sahihi ya vipodozi.

Hata hivyo, kuna njia rahisi ambazo zikifuatwa kwa makini zinaweza kumpa mwanamke muonekano bora na yenye mvuto.

Moja ya njia hizo ni ulaji wa matunda na mpangilio mzuri wa ulaji wa chakula kila siku.

Wataalamu wa urembo wanasema ulaji wa matunda unaboresha rangi ya ngozi na muonekano mzuri wa mtu husika.

Haya ni baadhi ya matunda yanayopendekezwa kama vyanzo vya virutubisho mwilini.

PARACHICHI: Tunda hili ni maarufu kutokana na kutumiwa kama juisi, lakini lina faida kubwa endapo utakula mara kwa mara.

Tunda hili lina vitamini za aina tofauti na huleta faida mwilini.Unashauriwa kula au kunywa juisi ya parachichi kila mara kama huna matatizo yoyote ya kuongezeka uzito.

APPLE: Tunda hili pamoja na kuwa na umaarufu duniani, pia lina maajabu katika kuweka ngozi katika uasilia wake.

Tunda la Apple lina vitamini na madini mbalimbali ambazo zina kazi ya kujenga na kukupa muonekano mzuri wa ngozi ya mwili.

NDIZI: Ulaji wa matunda aina ya ndizi husaidia kulainisha ngozi ya uso iliyokauka. Kutokana na umuhimu wake kuna baadhi ya mafuta yamechanganywa na tunda hili, ili kuongeza ubora wake. Ulaji wa ndizi urekebisha ngozi ya uso pamoja na kuupa uwezo mmeng'enyo wa chakula.

PAPAI: Ni tunda ambalo linasaidia kuipa ngozi mafuta, kurudishia sehemu zilizoumia na kung'arisha ngozi.

Papai lina enzyme inayoitwa papain ambayo kazi yake kubwa kuboresha ngozi. Pia tunda hili likichanganywa na asali, huwa 'scrub' nzuri ya uso kwani huleta matokeo ya haraka ya kusafisha na kulainisha ngozi.

CHUNGWA: Chungwa linasaidia kurudishia ngozi iliyodhurika na kuipa uhalisia wake.

Jinsi ya kutumia ni rahisi sana, chukua juisi ya chungwa ya baridi kisha paka usoni, acha kwa dakika 10, halafu osha hapo utaona matokeo yake.

Kwa msaada wa mtandao

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# SANDWICH ZA NYAMA YA HAM NA PARACHICHI

**Mahitaji:**
Silesi mbili za mkate.
Siagi kwa ajili ya kukaangia mkate.
Vipande viwili hadi vinne vya jibini.
Ham (nyama) vipande viwili kwa kila sandwich.
Nyanya.
Parachichi.

**Namna kuandaa**

Katakata nyanya na parachichi, weka pembeni.

Paka siagi mkate upande mmoja kila silesi, weka pembeni.


Weka kikaango katika moto wa wastani, weka mkate upande wenye siagi kwa chini.

Ongeza jibini (cheese) kwa juu ikifuatiwa na nyanya, parachichi na ham, kisa funika na jibini tena kwa juu.

Ongeza silesi ya mkate, upande uliopakwa siagi kwa juu.

Kaanga pande zote za mkate mpaka uwe wa rangi ya kahawia kiasi na jibini iyeyuke.

Pakua ikiwa ya moto kama utakavyopenda.



# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# UNATAKA KUJENGA? ANZA NAMNA HII



WAPENZI wasomaji wetu tumerudi tena baada ya mapumziko na tunaendelea na safari yetu Maisha ni Nyumba kukusaidia kupata ushauri na kuchagua ujenzi bora wa nyumba yako na mpangilio mzuri.

NI ukweli usiopingika kwamba kila mtu huwa na ndoto za kuwa na nyumba bora, katika kufikia lengo hilo, lazima kuwapo juhudi za ziada.

Kama ilivyo katika maeneo mbalimbali ya kutafuta maisha bora, pia ndivyo ilivyo katika kutafuta nyumba bora na wakati unapoona ndoto ya kulifikia hilo linakamilika, kuna umuhimu wa kuepuka makosa na majuto ya baadaye.

Leo darasa kuu ni kuangalia vitu vya kuzingatia kabla ya kuanza ujenzi wa nyumba bora, tukipata darasa kutoka kwa Msanifu Majengo, David Kashozi, anayetoa mwongozo kabla ya mtu hajaanza ujenzi.

Kabla ya ujenzi mtu anapaswa awaone wataalamu wamshauri, bila ya kujali ni aina gani ya nyumba unayotaka kuijenga.

Ushauri wa kwanza ni namna gani nyumba inatakiwa ikae kulingana na eneo la mtu.

Vitu vinavyopaswa kuangaliwa ni kama vile umbali unaotakiwa kujengwa nyumba kutoka kwa jirani yako.

Hapa unaangalia tahadhari ya majanga kama ya moto unapotokea kwa jirani usikuathiri kirahisi.

Vitu vingine vya kuangalia kabla ya kuanza kujenga, ni upangiliaji wa vyumba kwa ajili ya kuingiza upepo ndani.

"Kabla ya kuanza ujenzi kuna 'standard' (viwango) vya kitaalamu vya kuacha nafasi kutoka nyumba moja na nyingine, japokuwa tunaona baadhi ya watu wanajenga tu ovyo ovyo na mwisho wa siku, kunapotokea majanga kama ya moto, nyumba zote katika mtaa zinaungua," anasema Kashozi.

Mtaalam anaposanifu jengo anazingatia vitu vingi, hususani mwelekeo wa mahali ambako ni uelekeo wa upepo muda mwingi, pamoja na jua linakotokea na kuzama.

Kwa hiyo, ni vyema kuondoa woga hata kama hauko vizuri kifedha, kwa sababu kuna namna ya kukupata ushauri kulingana na hali yako ya kifedha.

# DONDOO MUHIMU ZA KUANDAA CHUMBA CHA KULIA CHAKULA

## MPANGILIO




1: Chumba cha kulia chakula cha kawaida kinatakiwa kuwa na nafasi ya kutosha ya kuweka meza na viti visivyopungua sita.

2: Chumba kinahitaji kuwa na meza moja kubwa katikati na kufanya kuwe na nafasi kubwa.

3: Viti vinatakiwa kuwa na mpangilio wa kuzunguka meza, viti viliwi ninawekwa kushoto na kulia, halafu kiti kimoja kimoja kila upande uliobakia.

4: Vitu vingine vya ziada vinavyohitajika kuwepo ni friji ndogo, kabati la vyombo, bomba la kunawia mikono, sofa ndogo kama ukipenda, taa ya juu yenye mwanga na meza ndogo ya kahawa au kuwekea vinywaji.


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
NAMBIE KISA CHA KUACHA KUNADI SERA ZA CHAMA CHENU NA KUANZA KUSIFU WANAWAKE?
UNADHANI KURA ZINAPATIKANA KAMA VOCHA?
JUKWAANI
HAJAFANYA LOLOTE 'ANAZUGAZUGA TU' KAMA UONGO ABISHE! HUYU HAMNA KITU!!
JAMANI KIZURI CHAJIUZA AU NAONGOPAAA?
JINSI YA KUNI-PIGIA KURA NI RAHISI SANA
RAHISI HIYO BILA KUSIKIA SERA ZAKO 'KWIO?'
MHESHIMIWA NIMEKUJA KUKUPA MBINU ZA USHINDI NISIKILIZE
USINITAFUTIE JAKAMOYO NA TAKUKURU NJOO MCHANA KWEUPEE
KUACHA KUSEMA TUKIKUCHAGUA UTATUFANYIA NINI NA KUANZA KASHFA INAKUWAJE?
KAISHIWA BANDO LA SERA
KILA SIKU UNANIAGA UNA-KWENDA KWENYE KAMPENI LAKINI SIKUONI JUKWAANI UNAKUWA WAPI?
MIMI MPAMBAJI
KUKATWA KUBAYA! YAANI NAPAONA KAMA UKWENI!
JIMBO
*KINYUNYIZO CHA LEO...
MGONJWA HAPONI KWA BIA...

HABARI KIMATAIFA

# UN yaonya nchi nne kukumbwa na njaa

**NEWYORK, Marekani**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, ameonya hatari ya kutokea baa la njaa katika mataifa manne ambayo yamekumbwa na migogoro ya vita duniani.

Kulingana na kiongozi huyo, mamilioni ya watu maisha yao yapo hatarini kwa tishio la kukosa chakula katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Yemen, Nigeria na Sudan Kusini.

Guterres, katika taarifa yake aliyoitoa kwa wajumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa mataifa, alisema mataifa hayo manne yanaongoza kuwa na matatizo ya ukosefu wa chakula.

Kauli yake hiyo, ilizingatia ripoti ya Dunia ya 2020, kuhusu mgogoro wa chakula na uchambuzi kuhusu usalama wa chakula.

Hata hivyo, alisema fungu la kuikwamua jamii katika maeneo hayo, bado ni dogo jambo ambalo limezidisha hofu.

**DW.**



Mwandamanaji wa Kipalestina akimfokea mwanajeshi wa Israeli, aliyesimama juu ya gari wakati wa maandamano yaliyofanyika karibu na Kijiji cha Naqura, Kaskazini Magharibi mwa Nablus eneo la Ukingo wa Magharibi jana. **(PICHA:AFP)**

# Uturuki yafanya mazoezi jeshi pwani ya Cyprus

**ANKARA, Uturuki**

UTURUKI imetangaza jeshi lake kuanza mazoezi ya kijeshi katika eneo la Pwani ya Cyprus, licha ya kuwapo na mvutano kati yake na Ugiriki.

Nchi hizo mbili zipo katika vita vya maneno kugombea eneo la bahari mashariki mwa bahari ya Mediterenia ambalo linaaminika kuwa na utajiri wa mafuta na gesi.

Katika taarifa ya Wizara ya Ulinzi, ilisema mazoezi hayo ya kila mwaka yameanza jana, ikiwa na lengo la kuboresha mafunzo ya pamoja, ushirikiano na kubadilishana uzoefu kati ya Uturuki na vikosi ambavyo viko katika eneo la kaskazini mwa kisiwa cha Cyprus.

Nchi hizo ambazo ni wanachama wa Umoja wa Kujihami wa NATO, kila moja inadai kuwa na haki ya kutafiti na kuchimba katika eneo hilo.

**DW.**

# Wanajeshi Mali wajadili kipindi cha mpito

**MALI**

UTAWALA wa kijeshi nchini Mali, jana ulifanya mkutano wa kujadili kipindi cha mpito kuelekea utawala wa kiraia.

Mkutano huo unafanyika baada ya kuwapo kwa shinikizo kutoka kwa nchi jirani ambazo zimetishia kuwawekea vikwazo kama hawatarudisha serikali ya kiraia.

Taifa hilo la Afrika Magharibi ambalo kwa muda mrefu limekuwa katika hali ya migogoro kutokana na kutokuwa na uthabiti, ghasia za kikabila na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Kundi la makanali waasi walipindua serikali na kumweka kizuizini Rais Ibraihim Boubacar Keita.

Mkutano huo ambao ulitakiwa kufanyika wiki iliyopita, uliahirishwa katika dakika za mwisho baada ya kutokea tofauti miongoni mwa wanajeshi hao na kundi la "vuguvugu la Juni 5 " ambalo lilikuwa mstari wa mbele kuandaa maandamano.

**DW.**

## India yafikisha visa mil.4 vya corona

**NEW DELHI**

INDIA imerekodi idadi kubwa ya watu walioambukizwa virusi vya corona na kufikia milioni 4, hadi jana na kulifanya kuwa taifa la tatu.

Nchi hiyo kwa sasa ipo nyuma ya Marekani na Brazil. Visa vipya vya maambukizi vimefikia 86,432 kwa siku mpaka jana.

Maeneo ambayo maambukizi yameongezeka kwa kasi ni mji mkuu wa New Delhi na majimbo mengine makubwa ya Maharashtra na Karnataka.

Ongezeko hilo la zaidi ya watu milioni 4 limetokea katika kipindi cha siku 13, baada ya taifa hilo kufikisha idadi ya maambukizi ya watu milioni tatu.

**DW.**

## Urusi yatangaza mafanikio chanjo ya corona

**MOSCOW, Urusi**

WANASAYANSI wa Urusi wamethibitisha kuwa chanjo yao ya virusi vya corona imeonyesha uwezo mzuri wa kupambana na ugonjwa huo.

Katika taarifa ya kwanza juu ya chanjo hiyo, wanasayansi hao walisema kuwa vipimo vya awali vimeonyesha ishara ya kuuwezesha mfumo wa kinga ya mwili kupambana na virusi.

Ripoti iliyochapishwa na jarida la kitabibu la The Lancet, ilisema kuwa kila mshiriki aliyepewa chanjo hiyo, aliweza kutengeneza sehemu ya protini ya damu inayoweza kuua virusi, bakteria na vimelea wengine hatari wanaoshambulia mwili wa binadamu na haikuwa na athari mbaya.

Urusi iliidhinisha chanjo hiyo na kuanza kutumiwa ndani ya nchi hiyo mwezi Agosti, mwaka huu ikiwa ya kwanza duniani kufanya hivyo.

Hata hivyo, baadhi ya wataalamu hao walisema majaribio yalikuwa ni madogo sana kuweza kuidhinisha ufanisi na usalama wa chanjo hiyo.

Utawala wa Urusi umesifu matokeo ya chanjo hiyo na kuyataja kama jibu kwa wakosoaji wake.

**BBC.**

## MAKALA

# Tuilinde amani kuelekea uchaguzi mkuu 2020



Na Magambo Masambu

TANZANIA ikiitwa Tanganyika ilipata uhuru Desemba 9 mwaka 1961 kabla ya kuungana na Zanzibar mwaka 1964 na kuwa Tanzania. Historia inaonyesha kwamba kabla na baada ya Uhuru, Tanzania imeongoza harakati za ukombozi barani Afrika na hasa nchi zilizoko Kusini mwa Afrika kuhakikisha zinapata uhuru wa nchi zao, amani pamoja na maendeleo ya kiuchumi.

Wanapotajwa viongozi mashuhuri katika harakati hizo hatuwezi kukwepa kulitaja jina la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama muasisi wa harakati hizo, kuhakikisha waafrika wanajitawala. Kwahiyo Mwalimu pamoja na viongozi wenzake wa Afrika wakahakikisha mapambano yatatulia tu pindi nchi karibu zote za Afrika zitakapokuwa huru na ikawa hivyo.

Tanzania kwa miongo kadhaa sasa imetambulika kama kisiwa cha amani. Inapotajwa mahali popote duniani picha ya kwanza ni amani yetu, taifa la watu waungwana, wenye utu, wenye kujali haki za wengine na utambulisho mkubwa ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, hata kama watu hawaifahamu nchi sawasawa unapomtaja yeye fikra zinakwenda kwenye harakati za ukombozi.

Sifa hii ya amani ambayo imekuwa ikitutambulisha kila mahali tunapaswa kuilinda kama msingi mkuu wa umoja wetu. Waswahili wanasema "Ukiona vyaelea ujuwe vimeundwa". Maana yake ni kwamba chochote kinachoonekana kina chanzo chake. Amani tuliyonayo kama taifa haikutokea tu tukawa nayo kazi na juhudi kubwa zimefanywa na viongozi wetu waliyotangulia, si jambo dogo kwa nchi kama yetu hii yenye makabila zaidi ya 120, kuwa pamoja, kuzungumza lugha moja kama Watanzania.

Nchi ambayo ina dini na madhehebu mbalimbali na kuheshimiana kwa misingi yetu ya imani, si jambo la kawaida sana kwani tumeona katika nchi nyingine wakitofautiana.

Wapo wanaofikiri kwamba sisi tumependelewa sana na Mwenyezi Mungu, lakini ukweli ni kwamba tulitangulia kupata viongozi wenye busara na hekima ambao walituweka pamoja kama taifa moja, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia viongozi wa aina hiyo. Kama amani hujengwa pia hubomolewa na watu na chenye kujengwa ili kiwe imara sharti kiwe kina msingi imara na msingi wa amani mahali popote huwa ni "Haki" haki ikitawala amani hutamalaki, haki inapovunjwa kuna uwezekano mkubwa pia wa amani kuvunjika.

Kuelekea uchaguzi mkuu 2020, kila mtu ndani ya nchi hii anawajibu wa kuhakikisha amani inakuwa zaidi ya uchaguzi wenyewe, kwani kuna maisha baada ya uchaguzi kwa vyovyote vile maisha lazima yaendelee.

Wanasiasa (wagombea) na wananchi (wapiga kura) matendo yetu katika kipindi hiki cha kampeni tunayoyasema na kuyatenda lazima yawe ni ya kujenga umoja wetu zaidi kuliko kutukosanisha, amani ikivunjika huvunjika kwa kila mtu na hakuna atakayebaki salama ni muhimu kuhakikisha amani yetu inakuwa kipaumbele katika matendo yetu sio maneno tu.

Wapo watu wanaodhani kwamba siasa haiwahusu kabisa na hawataki kusikia habari ya siasa, lakini ukweli ni kwamba siasa ni mfumo wa maisha haitamhusu marehemu tu, lakini tukiwa bado hai siasa inatuhusu kwasababu ndiyo mfumo unaotupatia viongozi wa serikali, hao ndiyo huamua namna gani ya kuendesha maisha yetu katika uchumi, elimu, biashara, kilimo, uvuvi, na mambo mengine yote, lakini pamoja na ukweli huu haimaanishi kila mtu ndani ya nchi hii ni mwanasiasa. Nafikiri wanasiasa hasa ni hawa wanaotafuta ajira majukwaani hivyo basi ni muhimu kutambua kwamba ajira hizi zisiathiri shughuli za wengine ambao wanajiona si wanasiasa japo siasa inawahusu, maana yangu ni kwamba mnaoomba ajira za siasa hubirini amani zaidi kwenye vinywa vyenu kuliko chuki na matusi.

Kwa upande mwingine ni wale wenye mamlaka ya kutoa haki, kama unajiona upo kwenye upande huu basi ni muhimu kuhakikisha kwamba haki mahali popote inatendeka na sio kutendekana tu bali ionekane kwasababu amani ni matokeo ya haki, usawa na ukweli tunaweza kuhubiri sana lakini tukishindwa kutenda mahubiri yetu yanaweza kuwa yananyakuliwa na ndege wa angani.

Sisi ni ndugu, tumeoleana tena bila kujali makabila yetu, rangi zetu wala imani zetu za dini, hatuna sababu yoyote ya kudhalilishana, kutukanana, kutwezana kwani baada ya uchaguzi Oktoba 28, 2020 inaweza kuwa ni aibu hata kutazamana. Madaraka ya kisiasa yasitufanye tuvuane nguo majukwaani hayo si mambo ambayo wananchi wanatarajia kusikia kutoka kwa wagombea. Wananchi wa Tanzania wanataka kusikia hatima yao ya leo, kesho na keshokutwa, wanataka kusikia sera nzuri zinazotokana na ilani za vyama vyao vya siasa hawahitaji kusikia mambo ambayo yatawajengea chuki na kuhatarisha amani yao.

"Now that you got what you wanted; you don't even know my name. Haya yamesemwa na mwana mziki nguli wa rege kutoka Afrika ya kusini Luck dube katika wimbo wake unaoitwa The Way It Is (jinsi ilivyo) kwa tafasiri isiyo rasmi sana anasema "Kwakuwa umepata kile ulichokitaka, hata jina langu hulijui tena". Katika vipindi hivi vya uchaguzi watu wengi sana hasa vijana hutumiwa kufanya uhalifu na maovu mengi ili kuhakikisha tu kwamba wale wanaowatuma wanapata madaraka.

Tunahitaji sote tupendane na tuwe wamoja, hatuna nchi nyingine bali ni Tanzania zaidi tuendelee kuilinda heshima ya nchi hii, majirani zetu wanatutazama tu kwasababu sisi mara zote tumekuwa walimu wao na wasuluhishi wao katika migogoro ya kisiasa, litakuwa jambo la aibu na fedheha kwa mwalimu kufanya mambo anayofanya mwanafunzi.

Amani ya Tanzania ni amani ya majirani zetu pia, utulivu wa Tanzania ni utulivu wa bara la Afrika, upendo wetu ni upendo wao pia hivyo lazima tukumbuke kwamba tunatazamwa kila mahali.

**Mungu ibariki Tanzania, ibariki Afrika na ulimwengu kwa ujumla.**

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mtoto wa Mwarabu mhamiaji aliyeitikisa nchi kwa muziki



Na Adam Fungamwango

MOJA kati ya matukio ambayo wakazi wa Morogoro na Tanzania kwa ujumla hawatoyasahau ni kuondokewa na mwanamuziki bora sana kitaifa, Salum Abdallah Yazid, maarufu 'SAY', hata ikaacha majonzi makubwa kwa mashabiki wa dansi Afrika Mashariki.

Ilikuwa Novemba 18, mwaka 1965, mwanamuziki huyo alipopoteza uhai tayari alishautwaa umaarufu mkubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Ni kifo cha ajali ya lori la mchanga alikokuwa akiliendesha, pale alipochomoka kutoka kwenye usukani ukawa mwisho wake, wapenda muziki wakiachwa katika majonzi mawazoni wana nyimbo zilizompa umaarufu mkubwa.

Hapo kuna vibao kama vile Ngoma Iko Huku; Shemeji Shemeji; Mkono wa Iddi; Wanawake Tanzania; Sipati Majibu; 'Naumia; Cuba Chacha; na Ewe Mola Wangu, ambao wachambuzi wengi wa muziki, wanakitafsiri katika sura ya utabiri wa kifo chake.

Alikuwa 'mboga saba'

Historia inaonyesha wanamuziki wengi wanatoka kwenye familia za kimaskini, lakini haikuwa kwa Salum Abdallah.

Yeye alitoka kwenye familia ya kitajiri. Baba yake, Mzee Abdallah Yazid, ana asili ya jamii ya Kiarabu kutoka nchini Yemen, aliyejikita mjini Morogoro, alikofunga ndoa na mwanamama wa Kitanzania.

Mzee huyo, alikuwa mfanyabiashara mwenye mafanikio kwa kumiliki migahawa kadhaa, maduka, magari madogo na makubwa, mjini humo.

Salum, aliyezaliwa Mei 5, mwaka 1928, alilelewa kwenye mazingira hayo ya vijana wa mjini kwa sasa wanayaita 'mboga saba', lakini kichwani alishatekwa na wito wa muziki ulioshika nafasi zote.

Tangu katika umri mdogo, Salum alipenda kwenda kwenye nyumba jirani zilizokuwa na mashine za santuri, maarufu 'rekodi pleya'.

Wakati huo nyimbo zilizovuma ni kutoka nchini Cuba, katika mitindo ya charanga, salsa, borelo zikiwa katika santuri zilizoitwa 'GV.'

Baba yake alimuweka Salum kwenye moja ya maduka yake, lakini mara nyingi alitoroka kwenda kusikiliza nyimbo hizo, kitu kilichomkasirisha sana mzazi, hata akamcharaza bakora kila mara. Mtoto hakukoma kiasi kwamba baba akaamua kubadilisha mbinu, aliamua kumnunulia 'pleya' ili kijana wake atulie dukani.

Hiyo kisaikolojia ikawa dawa, kwani Salum alitulia dukani na kufanya biashara vizuri, kiasi hata baba yake alifurahi na kuzidi kumpenda.

Baba alikerewa na uhalisia, akioona kijana wake kawehuka na muziki wa dansi, kwani itikadi yake kiimani haikukubaliana nayo hata kidogo.

Zengwe la rafikize baba

Hata hivyo, kitendo hicho kiliwakera baadhi ya marafiki wa Mzee Abdallah, waliomwambia mtu mwenye heshima zake kwa sifa za tajiri, muungwana na mwenye itikadi safi kiimani, haiwezekani mtoto wake apige muziki.

Ikumbukwe kuwa wakati huo muziki ulichukuliwa kama kazi ya watoto, umaskini na uhuni, huku Mzee Abdallah alikuwa Mwenyekiti wa Wazee wa Kiarabu Morogoro, hivyo ilionekana Mtoto Salum anadhalilisha, pia kuidhalilisha itikadi yao.

Baba yake aliungana nao, kwa sababu aliyakubali yaliyosemwa na rafiki zake, lakini katika sura ya pili alimpenda kijana wake na hakutaka kumkera, kwa sababu alionekana kuwa na akili ya kusimamia mali zao.

Hali hiyo ilisababisha kutoroka kwenda nchini Cuba, lakini meli iliishia Mombasa Kenya na pesa zilipomuishia alianza biashara ya kuuza mishikaki, hali aliporudishwa Morogoro na chama cha wafanyabiashara wa Kiarabu ambao tayari walishafahamu kuwa ni mtoto wa mwenzao mzee Yazid.

**KIFO CHAKE**

Ilikuwa Novemba 18, mwaka 1965, mwanamuziki huyo alipopoteza uhai alipokuwa amelazwa hospitalini, baada ya lori la mchanga alilokuwa akiendesha kupata ajali, ikiwa ni siku ambayo bendi yake ilitarajia kutumbuiza kwenye sherehe za kitaifa, ugeni mkubwa ulikuwa unasubiriwa katika mji huo.

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa, viongozi wakuu wa nchi wakati huo, walikuwa wakisubiriwa na wananchi wa hapa katika sherehe ya kufungua Chuo cha Kilimo ambacho kwa sasa kinajulikana kama SUA (Sokoine University of Agriculture). Pamoja na wageni hao pia alitegemewa kuwapo aliyekuwa Mbunge wa Morogoro mjini wakati huo Mheshimiwa Oscar Kambona.

Watu wakakesha na marehemu. Kesho yake hali ilizidi kuwa ngumu wakati wa kusindikiza maiti kwenda makaburini ilikuwa kama kila mtu alikuwa akitaka japo abebe kidogo jeneza, hadi ikalazimu FFU wawepo kuleta amani. Jeneza la Salum liliweza kubebwa kutoka Nunge nyumbani kwa mama yake hadi Msamvu kwenye eneo alipozikwa, watu wakiwa wamejipanga mstari mrefu, hakukutumiwa gari.

# HADITHI

DUNIA ina mambo mengine ya kushangaza sana. Unaweza kukuta baadhi ya mtu au watu wanaacha shughuli zao na kufuatilia ya wenzao, hata kama hawalipwi. Wanatumia muda mwingi kusema ya wenzao, huku yao wakiwashinda. Wengine ni watu wa karibu kabisa. Tatu, baada ya kuolewa na Rashid, yanamkuta ya kumkuta kutoka kwa mama mkwe wake, pamoja na jirani yake Zubeda. Alitamani ardhi ipasuke ajifukie chini. Fuatilia kisa hiki cha kushangaza.

# Mama Mkwe- 1

**Na Adam Fungamwango**
(0716 350534)




HII ni aibu mwanangu, unashindwa kwenda kazini, kazi yako unamfulia mwanamke nguo!" Mama Rashid alimbwatiza mwanawe, baada ya kuitwa aende uani akaangalie jinsi mwanawe Rashid anavyofua nguo.

Hakuwahi kuona hivyo, lakini alikuwa anaambiwa na Zubeda, dada mmoja anayeishi nyumba ya pili, ambaye wameunga urafiki na kuitana mama na mwana wa hiari.

Rashid, ambaye hakuwa na kipato kizuri, alikuwa bado akiishi nyumba ya mama yake, huku akiomba Mungu hali iwe nzuri, aondoke akapange na mkewe Tatu kwani alishajua kuwa mama yake ana mdomo na haelewani na mkewe.

"Kwani imekuwaje mama?" Rashid alionyesha kumshangaa mama yake, ambaye naye alikuwa anamshangaa yeye.

"We huoni tatizo ee?" Mama Rashid au Bi. Mwapewa aliuliza.

"Huyu keshalishwa limbwata mwanao huyu." Ilikuwa ni sauti ya Zubeda, ambaye ndiye aliyekwenda kumtonya Bi. Mwapewa kuhusu kijana wake kufua nguo wakati mkewe yupo ndani.

"Mambo unayoyafanya Rashid mbona hayafanani na wewe. Hii ni aibu unaniaibisha hata mimi mama yako," alizidi kumsakama kijana wake.

"Mama, mimi namsaidia mke wangu, kwani kuna kosa gani?" alijibu Rashid.

"Nimekwambia huyu mwanamke atakufanya uwe taahira, kwa nini humuachi? Mwanamke anakufulisha nguo, wewe unamng'ang'ania tu kama kupe." Bi. Mwapewa bado aliendelea kumpasha mtoto wake, huku povu likimtoka, akiwa ameshika kiuno huku Rashid akimwangalia mama yake kwa makini, akatikisa kichwa kwa masikitiko.

"Siyo kama ananifulisha mama, mimi namsaidia, kwani yeye si binadamu, anachoka na mume kumsaidia mke ni jambo la kawaida tu, wala siyo kesi," alijibu Rashid.

"Hivi mtu apige hodi hapa, akukute unafua, si unan'tia mimi aibu. Iwe mwanzo na mwisho." Bi. Mwapewa aliendelea kumsakama mwanawe Rashid.

"Mimi nitaendelea kumsaidia," alisema Rashid kwa sauti ambayo ilionyesha msimamo, kwani pamoja na kusemwa na mama yake mzazi, akishirikiana na binti wake wa hiari, bado hawakufua dafu kumshawishi aache.

**"Mimi nitaendelea kumsaidia," alisema Rashid kwa sauti ambayo ilionyesha msimamo, kwani pamoja na kusemwa na mama yake mzazi, akishirikiana na binti wake wa hiari, bado hakufua dafu kumshawishi aache.**

"Utafua sana mwaka huu." Sauti hiyo ilifuatiwa na kicheko cha kebehi kutoka kwa Zubeda.

"Wewe Zubeda na wewe mwisho wako unakaribia, nitakwenda kumwambia mumeo tabia yako siyo nzuri, unanidharau mimi kwa sababu umeungana na mama kumchukia mke wangu." Rashid aliongea huyu akimnyooshea kidole Zubeda.

"Kamwambie, kamwambie, kwani mimi namwogopa, loo, dume zima hata haya huna." Zubeda alijibu mapigo.

*******************************

Tatu Salum, awali alipoolewa na Rashid Jamal, alidhani kuwa maisha ya ndoa yatakuwa ya raha tupu. Pamoja na mama na bibi yake kumtahadharisha kuwa maisha ya ndoa yana tabu na raha, yeye aliona kama si kweli, kwani kabla ya kuingia kwenye ndoa, alikuwa na mchumba wake mzuri tu na kupendana sana.

Hakujua kuwa wakati mwingine kuingia ndani ya familia yoyote nako huwa na changamoto licha ya kwamba bado mtaendelea kupendana na mwenzi wako.

Sasa aliona taabu ya ndoa. Alivumilia na kuvumilia. Anampenda sana mume wake Rashid na anafahamu kuwa mumewe anampenda. Lakini kwa mbali akaona mwisho wa uvumilivu unakaribia kufika.

Siku moja ilipita baada ya tukio la mama mkwe wake Bi. Mwapewa kumjia juu mwanawe kwa sababu ya kufua nguo, ambayo yeye aliiona ni kama ametafuta sababu tu, kwani amekuwa akionyesha wazi kuwa hampendi.

Alifungua mlango wa chumba chake na kutoka nje. Barazani alimkuta mama mkwe na Zubeda ambao wanaonekana kuwa wameshibana na mara nyingi wengi hudhani kuwa ni mtu na binti yake.

"Simama hapo hapo kunguni we." Ilikuwa ni sauti ya Bi. Mwapewa ambaye alipomwona tu mkwewe Tatu alisimama.

"Mimi mama?"aliuliza Tatu.

"Sasa naongea na nani? Hivi we mtoto huna haya eee, kuamsha asubuhi asubuhi na kumfulisha mtoto wa mwanamke mwenzio minguo inahusu."

"Mi' sijamwamsha mama, wala sijamwomba, aliomba mwenyewe." Alijibu Tatu kwa sauti ya unyonge, upole na unyenyekevu.

"Mi Sijamwamsha mama, wala sijamwomba, aliomba mwenyewe." Bi Mwapewa alirudia maneno ya mkwewe, lakini kwa dharau, huku akiwa amebana pua.

"Kila kukicha kumfulisha mtoto wa mwanamke mwenzako nguo, we mtoto huna haya ee? Kwenu hakuna wakubwa. Toka umetia mguu wako humu ndani hakuna amani kwa ajili yako, unaogopa kwenda kwenu. Kwenu masikini eee." Bi. Mwapewa alizidi kushusha mvua ya maneno kqwa mkwewe.

"Mamaaa," bado Tatu aliendelea kumsihi mama mkwe wake kwa unyeyekevu na upole, licha ya kufokewa kama mtoto mdogo.

"Mimi sina mtoto kama wewe. Yaani niwe na toto limekomaa kama wewe. Najuta wewe ziraili kuingia kwenye nyumba hii." Bi. Mwapewa aliendelea kumsakama mtoto wa watu.

"Heheheheee, tenaaa..." Zubeda ambaye alikuwa kimya muda wote alicheka kizandiki.

"Nakwambia hivi, humu ndani utaondoka wewe. Hivi dunia nzima hujawahi kuona mwanamume kama Rashid? Hakuna eee. Bila Rashid huishi ee."

Maneno mazito aliyokuwa akishindiliwa mtoto wa watu, yalimfanya aangue kilio.

"Usinililie hapa. Kafa nani? Shangazi yako?

Tatu anaona yanazidi kuwa makubwa anakimbilia chumbani kwake na kufunga mlango na kuangusha kilio kwa sauti kubwa.

"Yaani ulivyomchamba sawasawa, haka kamwanamke kanaringa, shepu yenyewe hakana." Zubada alimgongea mama yake ya hiari huku wakigongeana mikono.

Mateso yaliendelea kumwandama Tatu. Siku mbili zingine baadaye akiwa bombani, alikutana na Zubeda. Kila mmoja alikwenda kivyake kuchota maji. Hakuna aliyeongea na mwenzake.

Zubeda baada ya kujaza maji yake, alijifanya anajitwisha, lakini anashindwa na kummwagia Tatu maji. Tatu alilowa, lakini hakusema kitu. Wakati baadhi ya kinamama bombani hapo wakidhani kuwa ilikuwa bahati mbaya, walisikia sauti iliyoashiria shari.

"Haya kwamwambie yeyote unayemtegemea kama mimi nimekumwagia maji."

Zubeda alitoa maneno hayo huku akiwa amejitwisha ndoo na kuondoka kwa namna ambayo ilionyesha kuwa ni mshari.

INAENDELEA JUMAPILI

## HABARI BURUDANI



## Pili Kitimtim anogewa penzi la babu

MSANII wa vichekesho, Pili Kitimtim, ameweka wazi maisha yake ya uhusiano, baada ya kusema anaishi na mwanaume mwenye umri wa miaka 52 kwa miaka 10 sasa.

Pili amesema suala la mapenzi halina umri, kwani licha ya kupitwa miaka mingi na mpenzi wake huyo, lakini wanaishi kwa furaha, upendo na yeye anamuona kama kijana sharobaro.

Ameeleza anachojali ni vigezo kutoka kwa mwanamume anayemtaka ambavyo ni awe mzee, mfupi, mnene na mweusi.

"Mimi nina mwanamume huu mwaka wa 10 sasa tunakimbizana hadi tunarogana tupo busy na uhusiano hatuachani leo wala kesho na kibabu changu hicho kina miaka 52 nakipenda sana, kwangu umri haunipi shida kwenye uhusiano ili mradi mwanamume awe mfupi, mnene, mweusi basi nachanganyikiwa"

# GIGY MONEY

## HATAKI UTANI ALIPA MIL. 4 KODI YA NYUMBA

MWANAMUZIKI wa BongoFleva, Gigy Money, amesema maisha yake yamekuwa mazuri kutokana na kazi anazozifanya na kukanusha kwamba hapati pesa kutoka kwa wanaume.

Akizungumza na Eatv hivi karibuni, Gigy Money, amesema ana pesa za kutosha ambazo zinamtosha kumlisha miaka mwili ijayo hata kama asipofanya kazi.

Amesema anakaa kwenye nyumba nzuri ambayo analipa yeye mwenyewe kodi ya Sh. milioni nne kwa mwaka bila kuomba msaada.

"Mimi ninafanya kazi zangu na najituma hakuna hata mwanamume nyuma yangu, msije mkajidanganya kama nadanga, ninalipa kodi ya milioni nne kwa mwaka, mimi sio mwanamuziki pekee bali ni mburudishaji, nina ushawishi na balozi nina pesa ambayo nimelipwa na zinaweza kunilisha miaka" amesema Gigy Money

## ALI KIBA KURUDI KATIKA MAISHA YA NDOA?

MAISHA ya mwanamuziki wa Bongo Fleva, Ali Kiba, mara nyingi yamekuwa sio wazi, amekuwa na tabia ya usiri kiasi ambacho si rahisi kujua kinachendelea katika familia yake.

Kutokana na tabia yake hiyo, hata ilipotokea mgogoro na mke wake, Amina Hlaef na kisha kutengana ilikuwa vigumu kufahamu, hadi hapo alipoamua mwenyewe kukiri.

Ali Kiba, kwa mara nyingine amesababisha mashabiki wake kuumiza vichwa vyao, baada ya jana kuweka picha katika ukurasa wake wa Instagram, ikimuonyesha yeye na mkewe wakiwa pamoja.


Picha hiyo imeibua mjadala mkali kwani mara ya mwisho msanii huyo kuwa pamoja na mkewe ilikuwa miezi mitano iliyopita.

Katika muda mfupi tangu iwekwe, mashabiki wengi walitoa maoni yao, huku baadhi wakimpongeza kwa kurudiana na mke wake ambaye wamebahatika kupata mtoto mmoja.

Ikumbukwe mara ya mwisho kwa nyota huyo wa muziki kuonekana na mkewe, ilikuwa kwenye siku ya kuzaliwa ya mtoto wao Keyaan, Februari 24, mwaka huu.



# DIAZ
## AJIUNGA MILAN KWA MKOPO



**MILAN, Italia**

BRAHIM Diaz amejiunga na AC Milan kwa mkopo akitokea Real Madrid kwa msimu wa 2020-21, klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A, imethibitisha.

Fowadi huyo mwenye umri wa miaka 21 alisajiliwa pale Madrid Januari 2019, lakini alishindwa kupata namba katika kikosi cha kwanza tangu atue kwa ada ya euro milioni 15 akitokea Manchester City.

Diaz alicheza mechi sita tu kwenye LaLiga msimu uliopita, huku zote akitokea benchi, na alikuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka.

Wakala wake, alithibitisha mazungumzo na Milan mapema wiki hii, akiishutumu Madrid kwa kutompa nafasi Diaz.

Licha ya kutokuwa kwenye mipango ya Zinedine Zidane, Diaz hajapata uhamisho wa kudumu, na ripoti zinabainisha kwamba Milan hawana kipengele cha kumnunua moja kwa moja.

Taarifa ya Milan ilisomeka: "Milan ina furaha kutangaza usajili wa mchezaji wa Hispania, Brahim Diaz kutoka Real Madrid kwa mkopo hadi Juni 30, 2021."

Diaz, alijiunga na Man City mwaka 2015 baada ya kuonesha kiwango cha kuvutia katika timu ya vijana ya Malaga.

## GREENWOOD APEWA JEZI NAMBA 11 MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

MASON Greenwood atavaa jezi namba 11 katika klabu ya Manchester United msimu huu, lakini namba saba bado haina mtu.

United ilitangaza Ijumaa namba mpya kwa wachezaji wao wawili waliotokea akademi yao, Greenwood na Brandon Williams kuelekea msimu mpya wa 2020-21 wa Ligi Kuu ya England.

Greenwood, ambaye jana Jumamosi alitarajia kuanza kuichezea kwa mara ya kwanza England dhidi ya Iceland, ameiacha namba yake 26 na kupewa namba 11 ambayo ilikuwa inavaliwa na gwiji wa United, Ryan Giggs.

Wakati huo huo, mlizi wa kushoto, Williams ameachana na namba 53 na kupewa jezi namba 33.

Lakini huku kukiwa na uvumi wa nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho kutua kikosinia hapo, United imeiacha namba saba ikiwa wazi, ikiwa imeachwa tangu kuondoka kwa Alexis Sanchez, Januari.

George Best, Eric Cantona, David Beckham na Cristiano Ronaldo wote walivaa jezi namba saba wakati wakicheza hapo United kwa nyakati tofauti.

Klabu hiyo tayari imemsajili Donny van de Beek kutoka Ajax ambaye amepewa jezi namba 34.

## COUTINHO ARUDI RASMI BARCELONA




**BARCELONA, Hispania**

PHILIPPE Coutinho amefanya mazoezi kwa mara ya kwanza na Barcelona, juzi Ijumaa baada ya kurudi kutoka Bayern Munich alikokuwa akicheza kwa mkopo.

Bayern iliamua kutomsajili kwa mkataba wa kudumu Coutinho, ambaye alitumia msimu wa 2019-20 na Bavaria hao kutokana na kuwa na wakati mgumu kule kwenye dimba la Camp Nou baada ya kusajiliwa kwa euro milioni 160 Januari mwaka 2018.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil amerudi kule Barca na ameanza kujifua kwenye maandalizi ya msimu mpya na timu, licha ya kuhusishwa na mpango wa kurudi Ligi Kuu ya England katika klabu ya Chelsea au Arsenal.

Coutinho alishinda Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, DFB-Pokal na Ligi ya mabingwa Ulaya wakati akiwa pale Bayern, akifunga mabao mawili na kusaidia moja wakati wa ushindi wa 8-2 dhidi ya klabu yake hiyo mjini Lisbon mwezi uliopita.

Barcelona kwa sasa ipo chini ya kocha mkuu mpya, Ronald Koeman.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# UAMUZI WA MESSI KUBAKI BARCA WAAMSHA SHANGWE

## ●●●Rais wa zamani na mgombea mpya wameshukuru kwa busara, lakini wasema...

**BARCELONA, Hispania**

MGOMBEA urais wa klabu ya Barcelona, Victor Font na rais wa zamani, Joan Laporta wamekaribisha uamuzi wa Lionel Messi kubakia kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina aliushtua ulimwengu wa soka wiki iliyopita baada ya kutangaza kwamba anataka kuondoka Barca siku kadhaa baada ya kutoka kuchezea kichapo cha mbwa mwizi cha mabao 8-2 dhidi ya Bayern Munich kwenye robo fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya.

Messi alitaka kuondoka klabuni hapo kama mchezaji huru, lakini miamba hao wa LaLiga walitaka kulipwa euro milioni 700 kama ilivyo kwenye kifungu katika mkataba wake.

Baada ya mvutano wa hapa na pale huku Messi mwenyewe akidai kufungu hicho kilishaisha muda wake Mei, Ligi Kuu ya Hispania ilitangaza kwamba kifungo hicho bado kipo hai.

Mapema juzi Ijumaa, Messi alithibitisha kwamba atabakia hapo kwenye dimba la Camp Nou.

Font, ambaye ndiye pekee wa urais wa klabu hiyo hadi sasa, awali alisema kwamba kuondoka kwa Messi ni "ndoto mbaya".

Lakini mara baada ya Messi kutangaza kubakia klabuni hapo, Font aliandika kwenye ukurasa wake wa Istagram kusifia uamuzi huo na kusema klabu hiyo imekosa mwelekeo kutokana na uongozi wa sasa.

Huku pia akionesha mipango yake kama akiutwaa uraisi atamchukua gwiji wa zamani wa klabu hiyo, Xavi kuwa kocha mpya.

"Hakujawa na mradi wa muda mrefu na hakuna chochote," aliandika Font: "Tunataka mabadiliko na tutaijenga upya klabu ya Barca. Ndio, kwa siku zijazo!"

Naye Laporta, ambaye alikuwa rais wa Barca kati ya mwaka 2003 na 2010 alisema uamuzi huo wa Messi mwenye umri wa miaka 33 kubakia klabuni hapo ni wa "busara".

Aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter: "Uamuzi wa Leo ni wa busara, ameelezea vizuri sana. Na sasa atarudi kupigania kushinda tena na kutengeneza historia. Leo Messi amewapa furaha zaidi mashabiki wa Barcelona!"

Uchaguzi wa rais mpya wa Barcelona utafanyika Machi mwaka 2021.

## KWA UFUPI

**KOULIBALY TAYARI KUONDOKA NAPOLI**

RAIS wa Napoli, Aurelio de Laurentiis, amesema mlinzi wa Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, ataondoka klabuni hapo kwa bei sahihi kipindi hiki cha majira ya joto, huku Manchester United na Manchester City zikiongoza mbio za kuwania kumsajili. ***(Talksport)***

**MAN CITY KUTOA OFA KWA KOULIBALY**

KLABU ya Manchester City inapanga kuweka ofa ya pauni milioni 66 kwa ajili ya kumsajili Kalidou Koulibaly wiki ijayo. (Inside Futbol)

**ABRAMOVICH ALIMSHAWISHI HAVERTZ**

MPANGO wa Chelsea kumshawishi kiungo wa kimataifa wa Ujerumani, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 21 kujiunga nao kutoka Bayer Leverkusen ulisimamiwa zaidi na mmiliki wake, Roman Abramovich kuliko kocha, Frank Lampard. ***(Express)***

**WERNER ALIKATAA KUJIUNGA MAN CITY**

MCHEZAJI mpya wa Chelsea, Timo Werner mwenye umri wa miaka 24 raia wa Ujerumani, alikataa nafasi ya kuhamia Manchester City baada ya kocha, Pep Guardiola kumpigia simu na kuzungumza nae ili amsajili. ***(Mail)***

**WEST HAM YAMUWANIA TARKOWSKI**

KLABU ya West Ham imetoa ofa ya pauni milioni 20 ili kumsajili mlinzi wa kati wa Burnley, James Tarkowski mwenye umri wa miaka 27. ***(Sky Sports)***

**DEPAY AMALIZANA NA BARCELONA**

KLABU ya Barcelona imefikia makubaliano ya kumsajili winga wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 26, kutoka Lyon. ***(Teamtalk)***

**MAN UNITED KUACHANA NA SANCHO**

MANCHESTER United inajiandaa kuachana na mpango wa kutaka kumsajili winga wa Borussia Dortmund na timu ya taifa ya England, Jadon Sancho kwa sababu wanahisi thamani ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 ni kubwa mno. ***(Star)***

**UNITED KUTOPUNGUZA BEI YA SMALLING**

MANCHESTER United pia haipo tayari kushusha bei ya pauni milioni 18 kwa mlinzi wake, Chris Smalling, mwenye umri wa miaka 30, lakini wana matumaini dili na Roma bado linaweza kufikiwa. ***(Corriere Dello Sport, via Star)***

**FRASER ATUA NEWCASTLE**

WINGA wa Scotland, Ryan Fraser, amewasili Tyneside kwa mazungumzo na Newcastle United. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 yupo huru kwa sasa baada ya kuondoka Bournemouth. ***(Sky Sports)***

**ARSENAL YAONGEZA KASI KWA PARTEY**

ARSENAL imetoa ofa ya wachezaji wake wawili raia wa Ufaransa, Matteo Guendouzi na Alexandre Lacazette ili kumnasa kiungo wa Atletico Madrid, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 27 raia wa Ghana. ***(Mirror)***

**ASTON VILLA WAKATALIWA KWA WILSON**

OFA ya Aston Villa kwa Straika wa Bournemouth, Callum Wilson mwenye umri wa miaka 28, imekataliwa. ***(Talksport)***



HABARI MICHEZO

# RC: Kaitaba itakuwa machinjio

Na Lilian Lugakingira, BUKOBA

MKUU wa mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, amezitaka timu za Ligi Kuu Tanzania Bara zitakazokwenda kucheza na timu ya Kagera Sugar katika uwaja wa Kaitaba zijiandae, maana hazitatoka salama katika uwanja huo, kutokana na kikosi cha timu hiyo kuwa imara zaidi.

Akizungumza wakati wa kukitambulisha rasmi kikosi cha timu ya Kagera Sugar, Gaguti alitangaza uwanjwa wa Kaitaba kuwa machinjio ya timu zote zitakazofika mkoani Kagera kucheza na timu hiyo.

"Tumedhamiria msimu huu, lazima tuwe mabingwa wa ligi kuu ya Vodacom, tumefanya maandalizi mazuri katika nyanja zote za kikosi na usafirishaji, ili wachezaji wetu wasafiri kwa raha," alisema.

Aidha alitoa ofa kwa mashabiki wa timu ya Kagera Sugar kuingia uwanjani bure katika mechi ya kwanza na ya tatu.

"Natoa ofa, mechi ya kwanza mashabiki 500 wataingia bure, mechi ya pili mashabiki 500 nao wataingia bure, lakini pia mechi ya tatu mashabiki 500 wataingia bure lengo kutia hamasa timu yetu," alisema.

Mwenyekiti wa chama cha soka mkoa Salumu Umande Chama aliwataka mashabiki wa Kagera Sugar kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu yao na kuwa shabiki ni nguzo ya ushindi.

Chama alisema Kagera Sugar itakuwa na mchezo wa kwanza ambao itacheza na JKT Septemba 07, mchezo wa pili itacheza na timu ya Yanga Septemba 19 na itakuwa na mchezo wa tatu na KMC Septemba 25.

Naye msemaji wa kiwanda cha sukari cha Kagera Vincent Mtaki alisema kuwa wanaitegemea timu ya Kagera Sugar kufanya vizuri katika msimu huu kutokana na maboresho ya kikosi yaliyofanyika.

Kocha mkuu wa Kagera Sugar Meck Mexime alisema kikosi chake kiko vizuri na kuwa wamecheza mechi za kirafiki na timu mbalimbali ikiwamo KMC, Mtibwa Sugar na Mwadui FC.

# WAAMUZI WAAHIDI HAKI LIGI KUU BARA

Na Adam Fungamwango

KAMATI ya Waamuzi nchini, imesema kuwa waamuzi wote wako tayari kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, na kuahidi watachezesha kwa kufuata sheria zote na kanuni zake, huku wakiwa fiti kimwili na kiakili.

Mwenyekiti wa Waamuzi, Sudi Abdi amesema kuwa wameshajipanga kuhakikisha wanapunguza matatizo yale yaliyokuwa wanajitokeza siku za nyuma na kuwatoa shaka mashabiki wa soka nchini kutarajia uchezeshaji wa hali ya juu.

"Tumewapa semina waamuzi wetu, tumewapima utimamu wa mwili, tumewafanyisha mazoezi uwanjani na darasani pia, tumewapima uelewa na pia tumewaangalia nyuma walifanya nini." alisema Sudi, mwamuzi wa Kimataifa nchini Tanzania.

Alisema kuwa mwanzo mwa Ligi Kuu wanatarajia kuanza na waamuzi ambao walifanya vema msimu uliopita.

Aliwahakikishia Watanzania kuwa makosa yatapungua kwa sababu na hata pale yatakapokuwa yanajitokeza, basi hawatosita kuyafanyia kazi.

"Waamuzi wako vema na watachezesha vizuri kuendana na wakati kwa sababu mabadiliko ya kanuni yao yanatokea mara kwa mara, lakini naamini kila timu kitakwenda vizuri," alisema mwenyekiti huyo.

Kuhusu kupata haki yao, Sudi alisema suala hilo haliko mikononi mwake, lakini akasema kuwa anaamini waamuzi watakuwa wanapata haki yao kama kawaida.

Ligi Kuu Tanzania Bara inaanza leo kwa mechi sita kupigwa, huku mechi tatu zikichezwa kesho Jumatatu.



Mgombea Ubunge Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA', akitumbuiza wakati wa kampeni ya kuomba kura kwenye Uwanja wa Jitegemee mjini Muheza. PICHA NA MPIGAPICHA WETU

# Mwana-FA ataja sababu ya kugombea Muheza

Na Steven William, MUHEZA

MGOMBEA Ubunge wa jimbo la Muheza mkoani Tanga CCM, Hamisi Mwinjuma maarufu kama Mwana-FA, amesema kuwa amesukumwa kugombea jimbo la Muheza kutokana na kero mbili.

Hayo yalisemwa juzi na mgombea huyo wakati akizungumza na maelfu ya wananchi wa Wilaya ya Muheza katika uwanja wa Jitegemee katika uzinduzi wa kampeni ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu wa 2020.

Mgombea ubunge huyo alisema kuwa kero kubwa ambazo ni maji na barabara ya kutoka Muheza mjini kwenda Tarafa ya Amani yenye urefu wa kilometa 35, ambayo ipo katika kiwango cha changarawe ambapo katika kipindi cha mvua huwa haipitiki.

Pia alisema atahakikisha anatetea mahitaji ya wasanii kwa ujumla akiwa bungeni kutokana na kuwa mmoja wa ati ya watungasheria hivyo

Kwa upande wake katibu wa Chama cha Mapinduzi CCM Wilaya ya Muheza, Mohamed Moyo, alisema kuwa wameshapatikana wagombea udiwani na ubunge sasa wale ambao wameshindwa kura za maoni waungane na wenzao ambao wameshinda kuwa kitu kimoja ili CCM iweze kushinda kushika dola.

Alisema kuwa kama kuna makundi ndani ya CCM katika Wilaya ya Muheza basi yavunjike mara moja ili kuhakikisha wanamuunga mkono mgombea ubunge jimbo la Muheza Hamisi Mwinjuma (Mwana FA) na madiwani ili upatikane ushindi wa kishindo na kwamba ufunguzi wa kampeni utafanyika tarehe 26 katika Tarafa ya Amani wilayani Muheza.

# Simba yaendeleza neema Sumbawanga

Na Adam Fungamwango

INAONEKANA kabisa kuwa mechi ya fainali ya Kombe la FA kati ya Simba dhidi ya Namungo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga imeendelea kuleta neema mkoani Rukwa, baada ya timu ya Mbeya Kwanza nayo kuamua kuelekea huko kwa ajili ya maandalizi ya Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Kocha Mkuu wa kikosi hicho Michael Mnyali alisema kuwa wanaamini Sumbawanga ndiyo sehemu sahihi kwao kwa ajili ya maandalizi.

"Tumeamua kuweka kambi mbali na familia za wachezaji ili wapate utulivu." alisema kocha huyo.

Kwa siku za karibuni Mkoa wa Rukwa, umekuwa na neema ya timu nyingi kukimbilia huko na hii ni baada ya mechi ya fainali ya Kombe la FA kati ya Simba dhidi ya Namungo iliyochezwa kwenye uwanja huo wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga na kufana mno, Simba ikitwaa kombe hilo kwa kushinda mabao 2-1.

Kufana kwa mechi hiyo na mwitikio wa mashabiki, hali ya hewa pamoja na uzuri wa uwanja wenyewe, uliivutia timu ya Ligi Kuu Prisons ya Mbeya ambayo imeamua kuhamia huko na kuufanya uwanja huo kuwa wa nyumbani.

Prisons ilipata mapokezi makubwa ilipotua Sumbawanga ikitokea Mbeya, ikionekana kabisa kuwa mashabiki wengi wanaweza kuwa wanajazana uwanjani timu hiyo inapocheza, kutokana na sababu nyingi, ikiwemo kutoona mechi za Ligi Kuu kwa muda mrefu.

Hali hii imeonekana pia kuivutia Mbeya City kwenda kuweka kambi mjini humo, ingawa haijatangaza kama itatumia uwanja huo, au itaendelea kucheza mechi zake kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya.

# Michezo

Jumapili Septemba 6, 2020

Nipashe




## Uamuzi wa Messi kubaki Barca waamsha shangwe

UKURASA 22

## Simba wapata CEO mpya

**Na Saada Akida**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Mohamed Dewj 'Mo' jana amemtambulisha rasmi Mtendaji Mkuu mpya wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez.

Akizungunza na waandishi wa habari jana, Mo alisema kuwa walikaa kwenye kikao cha bodi na kumteua Barbara kuziba nafasi ya aliyekuwa mtendaji mkuu wa timu hiyo, Senzo Mazingiza.

Mo alisema kuwa kutokana na vigezo pamoja na uzoefu aliokuwa nao bodi imeona ni vyema yeye akashika nafasi hiyo na anaamini atafanya vizuri.

"Tulikaa jana (juzi) kwenye kikao cha bodi na kumpendekeza Barbara kuwa mtendaji mkuu baada ya kuonyesha uwezo mkubwa pindi alipokaimu nafasi hiyo alifanya vizuri zaidi hivyo bodi ikapendekeza awe mtendaji wetu kwa sasa," alisema Mo.

Naye Mtendaji Mkuu, Barbara alisema kuwa amefurahi kupata nafasi hiyo na atahakikisha anaendeleza mazuri na mafanikio yaliyokuwepo.



Steven Bergwijn akishangilia bao lake la kwanza kuifungia timu ya taifa ya Uholanzi, wakati wa mchezo wa Ligi ya mataifa ya Uefa dhidi ya Poland uliopigwa kwenye Uwanja wa Johan Cruijff Arena jijini Amsterdam juzi. Uholanzi ilishinda bao 1-0. **PICHA NA MTANDAO**

# SIMBA, YANGA ZAANZA KUSAKA UFALME WA LIGI

### Kipenga chapulizwa leo, viwanja vyarindima, timu zajivunia vikosi huku...

**Isaac Kijoti, MBEYA na Adam Fungamwango**

KIPENGA cha Ligi Kuu Bara kimepulizwa rasmi na leo mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba watashuka dimbani kuvaana na Ihefu FC katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya, huku Yanga ikicheza na Prisons uwanja wa Benjamini Mkapa.

Simba itashuka dimbani ikiwa na morali ya hali ya juu, ikitaka kuendeleza mbio zake za ushindi baada ya kutoka kutwaa Ngao ya Jamii kwa kuifunga Namungo FC mabao 2-0 kwenye mechi hiyo ya kufungua msimu iliyopigwa Jumapili iliyopita katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Ushindi kwa Simba utatoa mweleko wa kuanza vema mbio za kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo katika mwezi huu wa Septemba ambao kwa mujibu wa ratiba ina mechi nne zitakazoiwezesha kuvuna pointi 12 endapo itashinda zote.

Baada ya mechi hiyo, Septemba 12, itashuka katika Uwanja wa Jamhuri Mjini Morogoro kuivaa Mtibwa Sugar kabla ya Septemba 20, kuialika Biashara United katika dimba la Mkapa jijini Dar es Salaam.

Septemba 26, Simba itahitimisha ratiba yake ya mwezi huu kwa kuialika timu nyingine inayocheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza, Gwambina FC ya Misungwi jijini Mwanza, mchezo utakaopigwa Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumzia maandalizi ya ligi hiyo, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amesema kikosi chake kipo tayari kwa mechi hiyo ya ufunguzi leo, lakini akaweka wazi ligi ya msimu huu itakuwa ngumu zaidi.

Sven amesema timu zote zinaonekana kujiandaa vizuri ikiwa ni pamoja na kufanya usajili wa kuvutia, hivyo kila mechi itakuwa ngumu, lakini anaimani upana wa kikosi chake utamsaidia kupata matokeo.

Kuhusu mechi ya leo, Sven alisema Ihefu ni timu ngeni katika ligi hiyo, lakini si ya kubeza, ila morali ya wachezaji wake na utayari wa mchezo unampa matumaini ya kuanza vizuri ligi hiyo.

Simba ambayo msimu uliomalizika wa 2019/20, imetwaa mataji matatu, Ngao ya Jamii, Kombe la Shirikisho (FA Cup) na Ubingwa wa Ligi Kuu Bara, imeimarisha kikosi chake kwa kusajili nyota wapya saba kuelekea msimu mpya wa 2020/21.

Katika safu ya ulinzi imeimarisha kwa kusajili mabeki wa kati wawili, Ibrahim Ame kutoka Coastal Union, Mkenya Joash Onyango mchezaji huru aliyemaliza mkataba wake Gor Mahia ya Kenya na beki wa kulia David Kameta 'Duchu' akitokea Lipuli FC.

Safu ya kiungo wa kati imemsajili Mzambia Rally Bwalya kutoka Lusaka Dynamos ya Zambia, huku winga ikimnasa Mghana Bernard Morrison aliyemaliza mkataba na Yanga.

Kwa upande wa safu ya ushambuliaji iliyokuwa chini ya Mnyarwanda Meddie Kagere na mzawa John Bocco, imeongezewa straika Mkongomani Chris Mugalu aliyejiunga na mabingwa hao akitokea Lusaka Dynamos pamoja na mzawa Charles Ilamya kutoka KMC FC.

Nyota hao ndio wanaomfanya Sven kujivunia kikosi kipana katika kila nafasi kutokana na uwezo binafsi wa kila mchezaji.

Kwa upande wake Yanga itaivaa Prisons kutoka Mbeya kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, huku wanachama na mashabiki wa timu hiyo wakiwa na matumaini makubwa na kikosi chao msimu huu.

Yanga itaingia uwanjani ikiwa na wachezaji wengi wapya, ambao watakuwa na kazi ya kuwaonyesha mashabiki wa klabu hiyo kuwa kikosi cha msimu huu ni moto wa kuotea mbali, kutokana na gharama kubwa zilizotumika kuwasajili.

Wanachama na mashabiki watakaokuwa uwanjani na kwenye televisheni zao, leo watataka kuangalia kiwango kama kile kilichoonekana kwenye tamasha la Wiki ya Mwananchi kwenye uwanja huo Jumapili iliyopita ilipocheza dhidi ya Aigle Noir ya Burundi na kushinda mabao 2-0.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kuwa maandalizi yote yamekamilika kwenye kambi yao iliyopo Kimbiji maeneo ya Kigamboni na kikosi kina majeruhi mmoja tu ambaye ni Mapinduzi Balama.

"Balama bado majeruhi na inawezekana akakosekana kwa muda wa wiki mbili, lakini wote 26 wako sawasawa, na Kocha Mkuu Zlatko Krmpotic ameniambia vijana wako tayari kwa ajili ya mchezo," alisema Bumbuli.

Kwa upande wa Prisons imesema kuwa Yanga wasitarajie mteremko kwenye mechi hiyo ili kuwafurahisha mashabiki wao.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ajabu Kifukwe, alisema kuwa kikosi chao kipo Dar es Salaam kwa muda mrefu kuisubiri Yanga.

Macho ya mashabiki wengi wa soka watakuwa kwa wachezaji wapya wa Yanga, hasa kina Tuisila Kisinda, Mukoko Tonombe, Michael Sarpong, Carlos Stenio Fernanders Guimaraes do Carmo Carlinhos na wengineo.

Mechi nyingine za Ligi hiyo ni Namungo vs Coastal Union, Biashara vs Gwambina, Mtibwa vs Ruvu Shooting na Dodoma vs Mwadui.

Lig hiyo itaendelea kesho wakati KMC itacheza na Mbeya City, huku Kagera ikiikaribisha JKT Tanzania na Azam kuivaa Polisi Tanzania.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >